

MAPITO YA NABII WA KWELI

 Asante, Ndugu Borders. Hebu tuendeleo tu kusimama wakati tukiomba. Sijui ni nani aliye na haja usiku wa leo, mngeweza kuinua mikono yenu na kusema, “Bwana, ni mimi”? Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

² Baba yetu wa Mbinguni, tunapousikia wimbo huo, “Bwana, naamini.” Tunaweza kuwaza juu ya—juu ya nyakati ambazo, kote ulimwenguni, nimeusikia huo katika lugha nyingi sana, “Bwana, naamini.” *Amini Tu*. Pia, Baba, tunaomba ya kwamba utakuwa ni zaidi ya wimbo kwetu usiku wa leo na uwe ni uhalisia. Jalia tuwe na imani kubwa Kwako usiku wa leo.

³ Na sasa tunaomba kwa ajili ya kanisa hili dogo, mchungaji wake, Ndugu yetu Fuller, mtumishi Wako, ndugu tuliye na imani naye. Nasi tunaombea familia yake, wafanya kazi wake hapa, mashemasi, wadhamini, na wote ambao huingia kwenye milango hii iliyobarikiwa. Tunaomba, Bwana, sikuzote litadumu mnara wa taa kwa ajili ya Yesu Kristo.

⁴ Wabariki ndugu wote wahudumu walio hapa usiku wa leo, wale wanaoingia na kutoka pamoja nasi, kote safarini. Tunaomba, Baba, ya kwamba Wewe utawabariki sana.

⁵ Nasi tunaomba, usiku wa leo, kwa ajili ya kumwagwa kwingine kwa Uwepo Wako juu yetu. Sisi ni wahitaji, Bwana. Tunakuhitaji Wewe. Sikuzote sisi ni wahitaji kwa kuwa tupo hapa kwenye uwanja wa vita, Bwana, ambapo maamuzi hayana budi kufanywa. Basi tunaomba, Baba, ya kwamba Wewe daima utatutia moyo kwa Uwepo Wako. Ina maana kubwa sana kwetu, kujua ya kwamba Wewe upo pamoja nasi. Jionyeshe tu Mwenyewe kwamba upo, Bwana, ndipo inatutia moyo kuendelea mbele. Ponya wagonjwa na wanaoteseka. Waokoe waliopotea. Watie moyo waliovunjika moyo. Jitwalie Mwenyewe utukufu. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

⁶ Ninaamini Daudi ndiye aliyesema, “Nalifurahi waliponiambia, ‘Na twende nyumbani kwa Bwana.’”

⁷ Billy alisema, muda mfupi uliopita, kasema, “Hivi kwa namna fulani si unachoka, baba?”

⁸ Nikasema, “Naam. Nimekuwa mchovu maisha yangu yote.” Ilifikia ambapo niliuzoea.

⁹ Nikaanza kuwazia, “Vema, ninakuwa mzee kupita kiasi. Inanipasa kupunguza kidogo angalau.” Ndipo mtu fulani akajitokeza, mwenye umri wa yapata miaka themanini ama tisini, anaichoma tu nchi moto, karibu mara mbili ya umri wangu, mwajua. Nikawazia, “Jamani! Ninajionea aibu.”

¹⁰ Huko chini maskanini nyumbani, kuna maskini mume na mke wazee jina lao Kidd, huja huko chini kutoka Ohio. Sasa, wote wawili wako ndani, mle ndani kabisa, themanini na mitano ama themanini na minane. Nao ni wazee sana hata hawawezi kwenda makanisani zaidi sana, kwa kuwa ninii yao... Hawana sauti ya kutosha. Lakini mnajua wanachofanya? Karibu kila kanda... Maskini mwanamke huyu mkongwe aliweka akiba pesa zake na kununua kinasasauti. Na kwa hiyo yeye huchukua kanda. Mimi humtumia kanda. Basi anazichukua kanda hizi, naye ataenda hospitalini, kila mahali ambapo anaweza kuweka kinasasauti hiki, yeye na maskini mume wake mzee, wakizicheza kanda hizo. Kisha nitamtumia jora kubwa la—la vitambaa vya maombi ambavyo nimeviombea. Na mara moja moja kila baada ya kipindi fulani, “Ndugu Willy, nimeishiwa na vitambaa vya maombi tena.” Halafu wakati ninapowaona, angekuja kanisani, maskini nywele zenye mvi, shali ndogo; naye mume, maskini jamaa mdogo.

Yapata miaka minne au mitano iliyopita, nilipokuwa kwenye...

¹¹ Mahali hapo panaitwaje kule Ohio, ambapo wanaufanyia ule mkutano kila mwaka? Wanapaita Chautauqua. Lakini ninasahau sasa. Ni uwanjani kule. Lakini li—lililo jina la mji huo, siwezi kulikumbuka. [Ndugu mmoja anasema, “Franklin.” Dada mmoja anasema, “Miami, karibu na Middletown.”—Mh.] Sasa, ni, mko karibu sana sasa. Mtu fulani alisema tunaenda moja kwa moja kupitia Miami. [Ndugu huyo anasema tena, “Franklin.”] Nao uko karibu na Franklin. Naam. Hiyo ni kweli. Papo hapo katika... Ninaamini ni kati ya Franklin... [Ndugu wawili wanasema, “Middletown.”] Middletown. Ndio huo. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, hiyo ni kweli, Middletown, huko chini mtoni, kwa hiyo kwenye viwanja vya Chautauqua mle ndani. Hapo ni kituo kile kikubwa cha mpira wa kikapu, cha riadha pale.

¹² Naye ndugu huyu, loo, nimewajua kwa miaka, na maskini mzee Ndugu Kidd ni, loo, nadhani ana themanini walipompeleka kule, nao madaktari wakakuta kwamba tezi kibofu chake kimekuwa cha kufisha. Na kwa hiyo kivimbe hiki kilimfunika kabisa. Vema, walisema hakina budi kufanyiwa upasuaji. Kwa hiyo walipomfungua, “Mbona, hakuna haja ya kumfanyia upasuaji. Yeye ni mahututi sana.” Mnaona? Kasema, “Hakuna njia ya kuufanya, hata kidogo.” Vema, akamleta maskini jamaa huyo nyumbani. Na, upasuaji huo, unamlema mzee huyo wa miaka themanini. Naye alikuwa na uzito tu wa yapata, loo, nadhani, chini ya pauni mia moja.

¹³ Kwa hiyo, Bibi Kidd akapiga simu, chini. Ndio kwanza nifike nyumbani kutoka mahali fulani. Ndugu Kidd alikuwa yuafa. Kisha kasema, “Anataka kukuona, Ndugu Branham, kabla hujanini... kabla hajaondoka.” Vema, mimi na Billy tulifanya zamu. Tuliupata huo—huo ujumbe, usiku mmoja, yapata saa

nne. Tukaanza safari, kesho yake asubuhi, kama saa kumi. Kwa sababu, aduhuri kesho yake, ilinibidi kuondoka tena. Nasi karibu tuzirarue taili za gari letu, tukienda kule.

¹⁴ Maskini mzee huyo, walimwamsha wakati nilipofika kule. Naye alikuwa na shali ndogo mabegani mwake, ameketi pale kama mzee wetu wa siku nyingi. Ilinifanyia jambo fulani. Basi nilipoenda kumwanguka, akatazama huku.

¹⁵ Palikuwapo na bikizee mwingine ameketi pale, aliyekuwa mmoja wa washiriki wa kanisa lake kwa kuwa yeye alihubiri milimani, nchi ya makaa huko Kentucky, ambako alifua kwa senti hamsini kwa siku, apate kumtuma mumewe huko hudumani kuihubiri Injili. Hiyo ilikuwa ni kama miaka kumi kabla sijazaliwa; akihubiri Ujumbe! Ndipo akaangalia huko, naye akamwita “nyanya,” huku yeye akiwa na umri wa miaka themanini. Naye bibi amepita tisini. Na kwa hiyo akasema, “Nyanya, unaonekana mweupe kama theluji.”

¹⁶ Nikawazia, “Hiyo ndiyo njia ya mhudumu kuwaangalia baadhi ya kusanyiko lake, wamelala, wameketi pale, wakifa. ‘Nyanya, unaonekana mweupe kama theluji.’” Naam.

Ndipo akatazama nyuma. Akasema, “Ndugu Branham?”

Nikasema, “Naam, Ndugu Kidd?”

¹⁷ Akasema, “Vema, nadhani haitachukua muda mrefu mpaka Yeye atakapokishusha gari langu chini.” Kasema, “Ninapaa juu, asubuhi ya leo.”

¹⁸ Nami nikasema, “Ajabu sana, Ndugu Kidd.” Nikasema, “Hiyo ndiyo njia ya kujihisi.”

¹⁹ Ndipo maskini Dada Kidd mkongwe, ni wangapi wanaomfahamu, hapa ndani? Naam. Ninajua, loo, wengi wenu mnawafahamu. Kwa hiyo akasema . . . Akasema, “Lakini, Ndugu Willy, hivi hufikiri Mungu angeweza kumponya papa sasa?”

Kasema, “Hakika, Yeye anaweza.”

²⁰ Naye akasema, “Vema, utukufu kwa Mungu!” Akasema, “Iwapo anataka kuniponya,” kasema, “ni—niko tayari kufanya kazi tena.”

Nikawaza, “Umri wa miaka themanini!”

Nikaanza kupiga magoti. Hapo likaja ono. Hilo lilitosha.

²¹ Siku mbili baadaye, wakamrudisha hospitalini. Wavulana wake walikuwa kwenye kikosi cha polisi pale mjini. Wasingeweza kulielewa. Wakamrudisha kwa daktari. Naye daktari akakuna kichwa chake, kasema, “Jamani, hakuna alama ya hicho ninayoweza kupata mahali popote, sasa, hebu nisimulie hadithi yako.” Ndipo karibu aivuruge hiyo hospitali. Akarudi moja kwa moja pamoja na kinasasauti chake, huyu hapa anakuja, akiucheza Ujumbe. Nao wanaishi kule kwenye . . . Na moja kwa moja kule karibu na Chautauqua na kule.

²² Sasa, mara ninapoanza *Ile Mihuri Saba*, kama tulivyofanya *Nyakati Saba Za Kanisa*. Alinipigia simu hivi majuzi usiku, kasema, “Vema, kipenzi, laiti ningalikuwa tu na pesa,” akasema, “hakika ningetaka kushuka nje.”

²³ Nikasema, “Sahau, Bibi Kidd. Na—nafasi yako inangojea. Wewe na baba shukeni mje.”

Akasema, “Nautakia heri maskini moyo wako!”

²⁴ Basi hilo linanifanya kujisikia vizuri sana, mwajua, maana wanania moyo. Kwenye umri wa miaka themanini na mitano ama themanini na sita, na wangali wanaendelea. Halafu mimi, ninanung'unika hapa, kwenye hamsini na mitatu. Kwa hiyo, jamani, inakufanya kujisikia kuwa na ushujaa.

²⁵ Vema, tuna mengi sana ya kuzungumzia, na kundi zuri sana la kuzungumzia, mbona, tungeweza tu kukaa hapa nusu usiku.

²⁶ Lakini inawapasa kwenda kwenye shule ya Jumapili asubuhi sasa. Sasa, inawabidi kufanya hivyo. Pia kumbukeni, daima nimesema, ni dhambi kabisa kuwatuma watoto wako kwenye shule ya Jumapili. Kamwe usifanye hivyo. Hilo ni kosa. Wapeleke, sikuzote. Mnaona? Sikuzote nenda pamoja nao. Yeye . . . Na kwa hiyo, sasa, hiyo ni asubuhi.

²⁷ Kwa hiyo, sasa, kama imekulazimu kukosa kwenda kazini, upate kusikia, kuwa pamoja nasi na kuomba pamoja nasi, na kadhalika, inakubidi kutoenda kazini, hilo ni sawa. Endelea tu ukose kwenda kazini, bali usikose kwenda kanisani. Usikose kwenda kanisani. Sitawachelewesha vya kutosha kukosa kwenda kanisani. Lakini ikikubidi kukosa kwenda kazini, mara moja moja, hilo halitadhuru. Sasa, maana, kazi, hicho ni chakula chako tu cha kila siku, na, wewe, Bwana aliahidi kukupa hicho. Kwa hiyo, lakini, hili, huna budi kuhakikisha kabisa umekuja kanisani. Unaona?

²⁸ Nafikiri, kesho asubuhi, niko pamoja na ndugu mwingine mwema hapa mjini. Ila sijui jina lake ni nani sasa. Nafikiri linaitwa Kanisa la Kimitume, ama Kanisa la Kimitume, hasa. Ni Kanisa la Kimitume. Hu—huenda nikamjua ndugu huyo. Jina lake haliko kwenye karatasi. Lakini si—sijui ndugu huyo ni nani kwa wakati huu. Halafu kesho usiku, huko juu . . . [Ndugu mmoja anasema, “Macias.”—Mh.] Ati nini? [“Ndugu Macias.”] Ndugu Macias. Loo, Macias. Loo, kanisa la Kimeksiko. Hiyo ni kweli? Loo, huyo ndiye aliyechukua mahali pa Ndugu Garcia wakati alipoondoka hapa? [“Kweli.”] Sawa. Hilo ni sawa kabisa.

²⁹ Aisee, nilipata barua, hapa siku moja, kutoka kwa binti yake, juu . . . Ndugu Garcia, huko juu Ca—California, angali anashikilia. Kwa hiyo, ninashukuru sana. Nami nilimwona Ndugu na Dada Garcia nilipokuwa huko San Jose, ninaamini, pamoja na Ndugu Borders huko juu. Wanaendelea tu vizuri. Kamwe sitasahau siku hizo usiku huko juu kwenye lile kanisa dogo la Kimeksiko. Kamwe sijapata kusikia “Gloria a Dios”

nyingi hivi maishani mwangu mwote. Kamwe sitasahau hizo, “Gloria a Dios.”

³⁰ [Ndugu Williams anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Jamani! Asante, Ndugu Williams. Hilo ni jema. Viti elfu moja mia tano, asubuhi, katika kanisa hili. Aisee, kila mtu aje huku, ikiwa hamwendi. . . Sasa, ngoja kidogo. Afadhali niwe mwangalifu kuhusu hilo. Nilisema kitu kibaya basi. La. Kwa uaminifu wote, unapasiwa mahali pako pa wajibu. Mnaona? Msininii. . . Sasa, hilo ni sawa.

³¹ Basi leo hii nilikuta kwamba wao. . . Niliona hema. Nilikuwa hapa chini kwenye ya Kumi na Sita na Henshaw. Ama, hivyo ndivyo ilivyokuwa nilipokuwa huku, huku Arizona, yapata miaka thelathini na mitano iliyopita, maskini barabara ya udongo. Nilienda huko nje mahali walipokuwa, na ilikuwa ni ya Kumi na Sita na Henshaw. Niliishi kule pamoja na watu fulani, Francisco, na—na sasa usingeweza kupajua mahali hapo. Hata wamebadilisha jina. Nafikri inaitwa Barabara ya Buckeye sasa.

Na, loo, jinsi mambo yanavyobadilika, lakini Mungu habadiliki.

³² Na kwa hiyo nilikuwa huko nikaona ndugu mmoja ana mkutano wa hema. Ndugu fulani huko chini aliyepiga hema. Nilienda kule kuona kama ningeweza kumwona, lakini sikumwona mahali popote, kumwambia ya kwamba hatukuwa hapa tupate kushindana naye. Lakini, kuna watu wengi sana tu hapa!

³³ Ninamkumbuka Jack Shuler. Hili lingekuwa zuri kwenu ninyi jamaa wa Kimethodisti. Wakati nilipokuwa hapa ndani wakati mmoja, ilikuwa ni huko Madison Square Garden, Jack alikuwa hapa nje kwenye—kwenye shule ya sekondari ya juu. Basi—basi nikampigia simu. Nami nikasema, “Ndugu Jack?”

Akasema, “Naam. Huyu ni Ndugu Branham?”

Nikasema, “Ndiyo.” Nikasema, “Nimekuvamia papa hapa.”

³⁴ Naye akasema, “La.” Kasema, “La. Nilikawia tu huku muda mrefu kupita kiasi hata nikaingilia wakati wako.”

³⁵ Nami nikasema, “Loo, samahani, Ndugu Jack.” Nikasema, “Sikuninii. . .”

³⁶ “Aa,” akasema—akasema, “hilo ni sawa, Ndugu Branham.” Kasema, “Walitaka tu nikae zaidi.”

³⁷ Nikasema, “Loo, kundi langu halitakusumbua huko nje, kwa vyovyote vile, Jack,” nikasema, “sababu karibu wangu wote ni Wapentekoste.”

Akasema, “Hakika, na wangu, pia.”

Nikasema, “Kweli?”

“Mbona,” akasema, “hakika.” Akasema, “Mimi ni mpentekoste.”

38 Nikasema, “Sasa, afadhali usimwache Bob ajue hilo.” Ni baba yake, mwajua. Naye ni Mmethodisti, pia, asiyepeleka mabadiliko, mwajua.

39 “Vema,” akasema, “Ndugu Branham, hivi hujui m—mpentekoste ni kitu gani?”

Nikasema, “Nafikiri ninajua.”

Akasema, “Ni Mmethodisti wa Kiorthodoksi.”

40 Hiyo karibu ni kweli, Mmethodisti wa Kiorthodoksi. Hiyo ni kweli. Kama kanisa la Kimethodisti lingaliendelea pamoja na ujumbe wake, lingeliingia moja kwa moja katika upentekoste. Ka—Kanisa halisi lilingia.

41 La, sio kulidharau dhehebu lenu sasa, ndugu. Mnaona? Kwa sababu, pentekoste si dhehebu. Walijaribu kufanya hivyo, bali hakika wameshindwa katika hilo. Mnaona? Ni tukio. Naam. Pentekoste ni kwa ajili ya Wakatoliki, ama—ama Wayahudi, ama mtu yeyote anayepata . . . Pentekoste ni tukio, sio dhehebu.

42 Na sasa kama kila mtu umeifungua Biblia yako, ama iko karibu, hata ungetaka kusoma pamoja nami Maneno machache. Napenda kusoma Neno, nanyi je? Kwa sababu, hata hivyo, yale ningesema yanaweza kushindwa, kwa sababu mimi ni mwanadamu. Bali yale Yeye asemayo hayawezi kushindwa. Mnaona? “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa.” Loo! Si ni ajabu hiyo? Neno Lake halitashindwa kamwe. Hilo ni jambo tukufu jinsi gani! Neno Lake halitashindwa kamwe.

43 Sasa hebu tusome usiku wa leo kutoka, na kutoa muktadha mdogo kutoka kwenye, lile nitakalochukua kwa ajili ya somo, Bwana akipenda. Liko katika Kitabu cha Amosi, unabii wa Amosi. Naye aliishi yapata miaka mia saba na . . . nafikiri ni karibu miaka mia saba na themanini na saba kabla ya kuja kwa Kristo. Hebu tufungue mlango wa 3 wa Amosi, Neno la Bwana kwa Amosi. Na mimi—mimi nampenda mtu huyu. Anachukuliwa kuwa mmoja wa manabii wadogo, bali hakika alikuwa na Neno la Bwana.

Lisikieni Neno hili alilosema BWANA, juu yenu, Enyi wana wa Israeli, juu ya jamaa yote niliowapandisha kutoka nchi ya Misri, nikisema,

Ni ninyi tu niliowajua . . . jamaa zote zilizo duniani; kwa sababu hiyo nitawapatiliza ninyi uovu wenu wote.

Je! Watu wawili wanaweza kutembea pamoja, wasipokuwa wamepatana?

Je! simba atanguruma mwituni, asipokuwa na mawindo? mwana-simba atalia pangoni mwake, ikiwa yeye hakupata kitu?

Je! ndege ataanguka mtegoni juu ya nchi, mahali asipotegewa tanzi? mtego utafyatuka juu ya nchi, bila kunasa kitu chochote?

Je! tarumbeta itapigwa mjini, watu wasiogope? mji utapatikana na hali mbaya, asiyoileta BWANA?

Hakika Bwana...hatafanya neno lo lote, bali huwafunulia siri zake watumishi wake manabii.

Simba ananguruma, ni nani asiyeogopa? Bwana MUNGU amenena, ni nani awezaye neno ila kutabiri?

44 Bwana na aongeze baraka Zake kwenye Maneno haya.

45 Hapana shaka maskini macho yake yalijifinya, wakati jua kali lilipoangaza asubuhi hiyo na kumeremeta ndevu zake zenye mvi na nywele zake, wakati akikipanda kilima kaskazini mwa Samaria na kuutazama ule mji. Mavazi yake kidogo yalikuwa ni ya kawaida, na miguu yake imejaa mavumbi. Hakutamanika sana kwa kuonekana, bali alikuwa na BWANA ASEMA HIVI kwa ajili ya hao watu.

46 Ni tofauti jinsi gani leo hii na uinjilisti wetu mamboleo! Ni mpangilio tofauti jinsi gani tulio nao, kuliko wake!

47 Maskini jamaa huyu, si mwingine ila Amosi, nabii wa kweli wa Bwana, akiwa na Neno la Bwana, kwa ajili ya kizazi hicho chenye dhambi! Maskini mtu huyu asiye na woga, alitabiri katika siku za Yeroboamu wa pili.

48 Yeroboamu alikuwa ni mtu mwerevu, mwerevu sana, mtu mwenye hekima, bali alikuwa ni mwabudu sanamu. Naye Yeroboamu alikuwa ameuongoza ufalme wake kufikia upeo wake, bali alikuwa katika ibada za sanamu. Alifanya hivyo kwa njia mbaya. Lakini huo ufalme ulikuwa umefanikiwa chini ya Yeroboamu.

49 Na, kwa kawaida, ufanisi husababisha dhambi. Watu wengi huangalia ufanisi kama baraka. Ungekuwa ni baraka, kama tungeweza kuutumia vizuri. Lakini kwa kawaida huongoza dhambini, kutokumheshimu Mungu.

50 Ufalme ulikuwa ukistawi katika siku zake. Pia, hao watu. Alikuwa amefanya ushirikiano na mataifa yote jirani.

51 Na jinsi ambavyo Israeli ilikuwa imepotoka ikaingia katika dhambi mbaya sana, ikamwacha Mungu, ikaziacha amri Zake na kanuni Zake, ikaenda kombo, kwa jumla, kwa mhemuko. Wanawake wakatembea mitaani, wamevaa nguo zao maridadi, zizizostahili. Wanaume wakatoka, wakicheza karata na kunywa pombe. Migahawa ya mitaani, tungeiita siku hizi, mahali pa burudani, pako wazi kabisa mjini.

52 Dhambi ilipuuza na huduma, imeanikwa tu wazi kabisa. Mahali pa kupendeza, kituo kikuu cha utalii, napo palikuwa

wazi kabisa. Dhambi haikukemewa kutoka mimbarani tena. Ilikuwa imeachiliwa kila mahali.

⁵³ Ndipo basi unabii huu ulipotokea, ilionekana kana kwamba usingeninii...Lingekuwa ndilo jambo la mwisho lingaliweza kutukia. Kulingana na yale nabii huyu aliyowaambia, litakuwa ndilo jambo la mwisho lingaliweza kuwapata, kutokana na vile yeye alivyokilaani kizazi hicho. Lakini, hata hivyo, chini ya miaka hamsini, ufalme wao ulikuwa umeangamizwa kabisa kutoka duniani.

⁵⁴ Mungu hunena Neno Lake. Nalo Neno la Mungu ni kama Mbegu. Basi inapopandwa, wakati nabii huyo alipokuja na Neno la Bwana na kunena maneno haya, ilibidi yatimie, kama yalikuwa ni Meneno ya Mungu. Wakati Ne—Neno la Bwana limetiwa mafuta, Nalo ni Neno la Bwana, Hilo halina budi kupachukua mahali Pake katika wakati Wake.

⁵⁵ Tunaweza kuliona, baada ya maelfu ya miaka, likipachukua mahali Pake siku hizi. Halina budi kuchukua, kwa sababu ni Neno la Bwana, na Hilo haliwezi kuangamia.

⁵⁶ Mtu fulani alikuwa akizungumza nami hivi majuzi, na kusema, “Mwanzo kimekosea, na zile siku sita za uumbaji, ambazo Yeye alisema.”

⁵⁷ Nikasema, “Mwanzo 1 hadi (Mwanzo) 2 ni kitu tofauti kabisa.” Mlango wa kwanza wa Mwanzo unasema, “Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi,” nukta. Jinsi alivyolifanya, na wakati alipolifanya, hiyo ni juu Yake. Naam. Halafu, “Nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu,” basi tunaanzia hapo, kwa ajili ya uumbaji. Lakini, “Hapo mwanzo,” umbali gani, sisi hatujui. Mbegu hizo zote alizokuwa nazo mle ndani wakati maji yalipoondoka, uhai ukarudi juu ya nchi tena, zikajiza dunia. Basi wakati Neno la Mungu linapopandwa, hakuna kitu kinachoweza kulizuia lisitendeke.

⁵⁸ Naye maskini nabii huyu asiye mwoga alitoka kusikojulikana. Jambo pekee tunaloambiwa kulihusu, ni kwamba alikuwa ni mchungaji. Hatujui baba yake alikuwa ni nani. Hatujui mama yake alikuwa ni nani. Hatujui aliko yeyote wa ukoo wake, hatujui lolote juu yake.

⁵⁹ Hivyo ndivyo kwa kawaida watu waliotumwa kutoka kwa Mungu wanavyojitokeza jukwaani. Wanatoka kusikojulikana, kisha wanatoweka vivyo hivyo. Hatukuwa na kumbukumbu yake kabisa, yaliyompata.

⁶⁰ Mtu huyu mashuhuri Yeroboamu, aliyekuwa bingwa ku—kuu la bongo, naye alikuwa ameliingiza taifa katika usitawi, hata hivyo, katika dhambi.

⁶¹ Nashangaa, kama tusingefananisha hilo kidogo na nchi yetu wenyewe, taifa letu wenyewe, katika dhambi jinsi lilivyo. Hata hivyo, ustawi, tutapunguziwa kodi, mara moja, nasikia.

Bila shaka, mtu yeyote anaweza kusoma katikati ya mistari pale, uchaguzi unakaribia. Lakini, kadhalika, mambo haya yote yanayoendelea.

⁶² Israeli, wahubiri, makuhani, na serikali walikuwa wameliacha Neno la Mungu nyuma, na kupatana. Na hiyo ndiyo sababu nchi ilikuwa katika hali iliyokuwamo, ingawa walikuwa na makuhani wengi tu, na wahubiri wengi tu kadiri ya waliopata kuwa nao. Bali walikuwa wameliacha Neno la Mungu, wakaliondokea. Na daima ni kwenye wakati huo, ambapo Mungu humtuma mtu kutoka pasipojulikana, kulilipua likarudi mahali pake tena. Mtu fulani asiye na woga atainuka pamoja na Neno la Bwana na kuwatikisa watu walirudie Neno tena.

⁶³ Nilikuwa tu nikiona hapa. Nilikuwa nimeandika kitu fulani hapa, ambacho ningetaka labda kukirejea tena. Hiyo ni katika mlango wa pili, kifungu cha 4. Ningetaka kulisoma. Msikilizeni maskini jamaa huyu akilinena hili waziwazi.

Haya ndiyo asema BWANA; kwa makosa haya matatu ya Yuda, naam, . . . manne, sitaizuia adhabu yake impate basi; kwa sababu wameikataa sheria ya BWANA, wala hawakuzishika amri zake, na maneno yao ya uongo yamewakoshesha, ambayo baba zao waliyafuata:

⁶⁴ Mnaona mahali ujumbe wake ulipokuwa? Kuurejesha moja kwa moja, kwamba walikuwa wameliacha Neno la Mungu. Kwa msomaji yeyote wa Biblia, hilo linakufanya ujue ya kwamba yeye alikuwa ni nabii wa kweli. Yeye aliwarejesha moja kwa moja kwenye Neno, ambapo walikuwa wameangukia.

⁶⁵ Loo, labda makanisa yao yalikuwa yamefanikiwa. Labda walikuwa na majengo mazuri. Mji wao labda ulikuwa maridadi kuliko Phoenix. Ulikuwa huko Samaria, kama sote tujuavyo, ulikuwa ni kituo kikuu cha watalii. Hata sasa, bado ungali ni mahali pa kupendeza.

⁶⁶ Lakini, hata hivyo, walikuwa wamemwacha Mungu. Ndipo Mungu akawatumia huyu mjumbe. Ni ujumbe wa kemeo jinsi gani kutoka kwa Mungu! Maskini nabii huyu aliwatoa.

⁶⁷ Sasa, Amosi alitoka nyikani, akaja kwenye mji wa madoido. Si ajabu maskini macho yake aliyopewa na Mungu yalijifinya wakati akikipanda kile kilima. Yeye . . .

⁶⁸ Sio kama vile mtalii angefanya, enyi kina mama, tuseme, "Tazama ununuzi wote ambao wanawake wanafanya. Angalia mitindo mipya waliyo nayo hapa chini," ama sio kama vile baadhi ya wanaume wangewazia, "Yale makasino, na kadhalika, yalikuwa ni maarufu sana mjini," ama kwa sababu kwamba huenda wakaketi pembeni mwa mtaa na kuangalia wale wa hiyo jinsia nyingine wakipita, kuwatamani.

⁶⁹ Lakini nabii huyu, macho yake yalijifinya kwa sababu ya dhambi alizoonza mjini. Hayakuwa yakijifinya kwa sababu ya mambo aliyokuwa akitamani, bali ni kuona jinsi walivyokuwa wamemwacha Mungu kwa mbali, watu waliokuwa wameitwa na kuchaguliwa. Hivi mliona hapa? Yeye alisema, “Siwajui watu wengine ila ninyi. Niliwatoa Misri, halafu mnaniacha namna hiyo.”

⁷⁰ Basi wakati nabii huyu, akija kutoka kwa mchungaji hadi kwenye nchi ya kaskazini, akiwa na Neno la Bwana, jinsi alivyouangalia mji huo. Hapana budi alifuta jasho. Nguo zake zilikuwa ni mbovu. Na labda hana pesa za kutosha kukodi chu—chumba kwa ajili ya usiku huo. Haikuleta tofauti yoyote kwake. Alikuwa na ujumbe uliokuwa ukiwaka moyoni mwake, na hana budi kuuleta. Sio hivyo tu, lakini upako wa Roho Mtakatifu uliokuwa umemgusa huko nje nyikani, ulikuwa umeyafumba macho yake yasiyaone mapambo ya ulimwengu.

⁷¹ Na mtumishi yeyote wa Kristo aliyetiwa mafuta, macho yao yamepofushwa yasiene mambo ya ulimwenguni. Hawayaoni mambo hayo. Hawayatafuti. Wanalo jambo moja: Kristo yuko mbele yao. Hilo tu ndilo wanaloliona. Hawaogopi chochote. Kristo yuko mbele yao. Ujumbe hauna budi kupelekewa watu, na hakuna kitakachowazuia. Huwezi kuchoma Huo ukawatoka. Unaweza kuwafunga jela, korokoroni, chochote utakacho. Watatoka moja kwa moja humo tena. Hao ni watiwa mafuta wa Bwana. Naam.

⁷² Yeye aliangalia uozo wa kiroho wa mji huo, utovu wa uadilifu, na uozo wa kiroho wa mji huo.

⁷³ Nashangaa ni watumishi wangapi wa Bwana, wanaovuka juu ya huu mlima hapa juu, wangeangalia Phoenix? Mnakuja hapa kwa ajili ya mapambo, na kuota jua, na kustarehe, ambalo hatuwezi kulidharau hilo.

⁷⁴ Hapa si muda mrefu uliopita, wakati wa mwisho nilipokuwa hapa, nikiketi juu ya Mlima wa Kusini, mke wangu anayeketi pale nyuma, nilikuwa nikizungumza naye. Nikasema, “Yapata miaka mia tatu ama mia nne iliyopita hili bonde lilikuwa ni mahali pazuri, hapana shaka, wakati Mto wa Chumvi ulipopitia hapa, na mbwa mwitu, na kadhalika, na kuchanua kwa mipungate. Angalia jinsi limeninii...Kitu hicho chote kimekuwa ni mkusanyiko wa dhambi.”

Naye akasema, “Vema, basi ni kitu gani kinachokuleta hapa?”

⁷⁵ Nikasema, “Hili hapa linalonileta hapa. Ingawa katika giza lake na katika dhambi iliyo kwenye huu mji, kuna shuhuda fulani za Bwana, mifano iliyo hai ya Kristo, huko chini. Ninakuja kuungana nao, kuiangaza Nuru ya Injili. Baadhi ya maskini ndugu hao huko chini pembeni mwa barabara mahali fulani, waliifanyia kazi, na kujitahidi sana, na kulia na kuzama katika

maombi, wakiwa na ujumbe moyoni mwao. Ninakuja kujumuika nao, kuangaza Nuru ya Injili isiyoghoshiwa ya Yesu Kristo kwenye eneo hili la jimbo la mji huu wa Phoenix.”

⁷⁶ Wenyewe, hata hivyo, ungekuwa ni mahali pazuri sana; kama mtu angeweza tu kuchukua ufanisi wake ambao ameweza kupata, kujenga makazi mazuri kama yaliyo juu ya Mlima Camelback, Mlima Cavalier. Kama vile nilivyopitia pale, mbona, miaka thelathini na mitano iliyopita, hapo palikuwa ni jangwa. Tuliwakimbiza punda wadogo kule kwa mgongo wa farasi. Na huko juu ya Mlima Kusini hapa, tukiwakimbiza punda wadogo na farasi.

⁷⁷ Na sasa umekuwa ni eneo kubwa la jimbo la mji huu wa kupendeza mno. Unastawi upate kuenea makumi elfu mara maelfu. Umepanuka, mpaka sasa uozo wenyewe wa miji unauingiza katika machafuko. Ukungu na moshi unaingia. Unyevu wenu ni mbaya kama ulivyo Jeffersonville, Indiana, kwenye Bonde la Ohio. Unyunyiziaji... Mwanadamu daima huuchafua ulimwengu. Wakati Wahindi walipokuwa hapo, palikuwa ni mahali pa kupendeza. Bali wakati mzungu alipoingia, alileta dhambi zake, na pombe, na utovu wa uadilifu. Naye amechafua nchi mpaka imekuwa si kitu ila karibu ni shimo la takataka. Ni kitu cha jinsi gani kuangalia! Mungu atakifagilia mbali kutoka kwenye uso wa dunia, moja ya siku hizi.

⁷⁸ Naye anawachagua watu, katika haki, ambao watatawala juu ya nchi, wakati Yeye akitawala kama Mfalme. Sasa Yeye anawachukua watu kwa ajili ya Jina Lake, watu kwa ajili ya Ufalme Wake.

⁷⁹ Sasa, kundi hili erevu, lenye akili, la wasomi wa Israeli; rais ama mfalme wao mkuu, mwenye nguvu, Yeroboamu, aliyekuwa ni mtu mwenye akili; na hivi wao wangemsikia maskini nabii huyu, asiyejulikana? Ujumbe huu mkuu, unaowaka moyoni mwake, hivi angeweza kutembea mitaani, nao watu waweze, wanawake waweze, kuvalia vizuri tena, wanaume waviache vilabu vya pombe na mahali pa dhambi, na kumgeukia Mungu kwenye mahubiri ya maskini jamaa huyu, asiyejulikana? Hilo ni swali huenda lilikuja niani mwake, ama linalokuja niani mwangu, ninapomwona amesimama pale, na maskini kichwa chake, chenye upara kiking'ara kwenye jua. Ndevu zake zenye mvi zikining'inia kwenye koti lake. Akiangalia chini kupitia pale, na kuuangalia mji huo, nayo macho yake yanajifinya, huku moyo wake ukidunda.

⁸⁰ Na hata hivyo, humo ndani, yeye aliuona Ufalme wa Mungu, ambao unapaswa kuanzishwa kule, wote umelemewa na dhambi. Na pamoja na shutuma kutoka kwa Mungu, ambalo litashutumu kuanzia mfalme hadi ombaomba mtaani, kila kuhani, mhubiri, mfalme, mtawala, mtawala mkuu, chochote alichokuwa, alikuwa na laana ya Mungu kuwawekea

juu yao. Kwa sababu wao... Ungewazia wangempokea. Loo, wangepahamu hilo?

⁸¹ Kumbukeni, yeye hakuwa na pendekezo lolote. Alijitokeza tofauti na wainjilisti wetu wa siku hizi. Yeye hakuwa na pendekezo lolote kutoka kwa makuhani. Hata hawakujua huyo jamaa alikuwa ni nani. Lakini kulikuwako na Mmoja aliyejua yeye alikuwa ni nani. Huyo alikuwa ni Yule aliyemtuma. Hilo tu ndilo lililojalisha, kwake, mradi tu alijua alitumwa kutoka wapi. Ujumbe wake ilibidi uendeleo hata hivyo, na pasipo kujali.

⁸² Hakuwa na utambulisho wa kimadhehebu wa kumuunga mkono wakati alipoingia mjini, kuja kwenye shirika la wahudumu, kusema, "Ndugu zangu, nimetumwa na kundi fulani *hili*, kundi hili la dini. Mimi ni mfuasi wa *fulani-fulani*." Hakuwa na hilo. Hakuwa na chochote cha vitu hivyo. Wala hakuwa na kadi ya ushirika ya kuonyesha alikuwa na ushirika mwema pamoja na shirika la wahudumu kutoka kwenye nchi alimotoka. Hakuwa na ushirikiano kwa kampeni yake. Hata hakumtaka shauri mtu yeyote kuhusiana nayo.

⁸³ Maskini jamaa huyo alikuwa amesimama mahali pagumu. Ingetosha kwa mtu kugeuka na kurudi, na kuwarudia mifugo wake tena, aanzie mahali alipoachia, kama tu angeliwazia.

⁸⁴ Lakini, mnaona, mtu huyo hakuchukua wazo lolote la pili. Hakuwazia juu ya utambulisho wowote, wala hakuwazia juu ya kadi ya ushirika. Yeye aliwazia tu jambo moja, na hilo lilikuwa ni Neno la Bwana. Mungu alikuwa amempa Hilo pamoja na agizo, ya kwamba hana budi kwenda kule na kutabiri. Hilo tu ndilo lililoleta tofauti yoyote kwake. Alikuwa na Neno la Bwana, na kwa hiyo alijisikia hakuhitaji utambulisho wowote, wala idhinisho lolote, wala ushirikiano wowote. Kitu pekee alichohitaji, kilikuwa, alikuwa na ushirikiano na Mungu, na hicho tu ndicho kilichohitajika. Mradi tu alikuwa katika mapenzi ya Bwana, ilileta tofauti gani? Mradi tu alijua ya kwamba ujumbe wake ulikuwa umetoka kwa Mungu, Mungu angehibitisha ujumbe huo. Ilibidi ahibitisha.

⁸⁵ Ndipo alipouleta ujumbe, inaonekana kana kwamba kungekuwako na makuhani wote, na wahubiri, na manabii wa wakati huo, wangekuja na kutubu, kwa sababu wangekuwa wameona hali ya mahali hapo, kuona kudorora kwa maadili. Lakini wakati alipoanza kutabiri kwa Neno la Bwana, Hilo lilikuwa ni geni kwao. Hawakujua lolote kulihusu Hilo.

⁸⁶ Hiyo ni picha nzuri sana ya siku hizi. Ni mgeni, ujumbe wa Bwana! Kanisa halijui chochote kuuhusu. Wanapowasikia watu wakisimama na kutoa ujumbe kwa lugha zisizojulikana, na kutoa tafsiri yake, na kusema jambo fulani liko karibu kutukia, watu wanageuza kichwa chao na kuondoka; wanafikiri hao watu wana kichaa. Wanamwona mtu akisimama katika Roho na kutabiri, ama kutoa ujumbe kutoka kwa Bwana, mbona, watu

wa ulimwengu wa kanisa leo hii wanawazia mtu huyo amerukwa na akili zao. Ni ngeni kwao, kwa sababu karibu wako kwenye hali ile ile, leo hii, kama Samaria ilivyokuwa siku ile.

⁸⁷ Lakini, kumbukeni, mataifa yanapofikia, ama kanisa la Mungu sikuzote lilipofikia hali hiyo, Mungu aliweza kumwinua nabii akiwa na Neno la Mungu kwao. Bila shaka.

⁸⁸ Walikuwa wamelisahau, muda mrefu uliopita. Lakini walipaswa kukumbuka, pasipo kujali kama wangeweza kuchunguza kwenye vitabu vyao, waone kama walikuwa na jamaa fulani kutoka kwenye baadhi ya shule zao, jina lake Dk. Amosi, ama sivyo. Walipaswa kujua, ya kwamba, “Mungu wa Ibrahim aliweza kutoka kwenye mawe haya kuwainua watoto, ama manabii, kulileta Neno Lake.”

⁸⁹ Naye Mungu yuyo huyo anaweza tu usiku wa leo kama alivyokuwa wakati huo. Nalo lingeninii, hakika, alifahamika vibaya na watu. Yeye anaweza kuwainua watu, awatie watu mafuta, kulileta Neno Lake. Yeye anaweza kuliweka Neno ndani ya mwanadamu, akamtuma, na kuthibitisha ya kwamba Yeye ni Mungu, kwa mtu huyo ambaye atajinyenyekeza mwenyewe na kujitiisha kwa Mungu, na asiogope kwenda na kuliamini Neno Lake Mungu. Yeye anaweza kufanya hivyo, na Yeye atalifanya. Aliahidi atalifanya.

⁹⁰ Nayo Maneno Yake, hakika, yalithibitishwa kwao katika siku hiyo. Kwa sababu, wakati kizazi hicho hicho kilipokuwa kingalipo, yote ambayo Amosi alitabiri yalitimia.

⁹¹ Nashangaa leo hii, sasa, kwamba kama Amosi angekuja kwetu, hivi tungempokea leo hii? Phoenix ingempokea Amosi? Kama mahali fulani upande wa pili wa mlima hapa, mahali fulani, ama huko chini kutoka sehemu fulani ya nchi, angetokea maskini jamaa mdogo, mwenye nguo mbovu namna hiyo, aje hapa na kuwahamasisha wahudumu, na kusema, “Ninalo Neno la Bwana,” mnafikiri tungempokea? La hasha.

Jambo la kwanza tungemwuliza, “Uko pamoja na kundi lipi?”

⁹² Basi vipi kama angegeuka, aseme, “Kundi la Mbinguni”? Hilo kidogo lingekuwa ni la kigeni kwetu, nahofia.

⁹³ Lakini hivyo ndivyo ilivyokuwa wakati huo. Na labda ingekuwa vivyo hivyo siku hizi kama Amosi angalijitokeza jukwaani.

⁹⁴ Hebu, kwa ajili tu ya yale nimesema, tumlete hapa, kwa dakika chache tu, na tuone kile tunachowazia yeye angefanya. Mnajua kile angefanya? Ninaamini angetofautiana na mpangilio wetu wote. Naam, bwana. Angetofautiana na mafundisho yetu ya kimadhehebu. Angewahukumu Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Lutheri, Mkatoliki, na Wapentekoste. Angekiingiza kitu hicho chote ndani. Hakika angekiingiza.

Angetofautiana na mafundisho yao ya kimadhehebu. Angeenda moja kwa moja kwenye msingi asili wa Neno, na kuanza moja kwa moja kwenye Neno. Angeanza kampeni yake juu ya BWANA ASEMA HIVI.

⁹⁵ Mbona, mbona, mnafikiri Phoenix ingempokea? Mnafikiri Louisville ingempokea; New York, Boston, Massachusetts, ama chochote kile, California? La, bwana. Wangemtia maskini jamaa huyo gerezani upesi wangiweza kumtia mle. Bila shaka wangemtia. Hakika wangepanya hivyo. Kama angelirejea kwenye Neno, nina hakika wangemtia gerezani, maana kila kundi lisingekubaliana naye. Kusingekuwako na mmoja angalikubaliana naye, maana hawana budi kushikilia mapokeo yao kusudi wasikubaliane na Neno.

⁹⁶ Ingetubidi kukumbuka kwamba yeye ni nabii wa kweli. Kama angalikuwa, na kama alikuwa nabii aliyetumwa kutoka kwa Mungu, angekuwa na alama moja kwake, alama moja dhahiri ambapo tunajua yeye ni nabii: angedumu na Neno. Maana, hapo ndipo Neno la Mungu lilipokuja, ilikuwa ni kwa manabii.

⁹⁷ Unajua yale angefanya? Angekilipua na kukihukumu kizazi hiki. Angemhukumu kila mwanamke aliyekata nywele zake nchini. Angemhukumu kila mhubiri wa kimadhehebu. Hakika angefanya hivyo. Angemhukumu kila mvuta sigara, kila mwanamke aliyevaa kaptura ama suruali ndefu. Angewararua vipandevipande. Kwa nini? Ni kinyume na Neno. Kweli kabisa.

⁹⁸ Mnafikiri tungempokea? La hasha. Wasingempokea.

⁹⁹ Angemhukumu utovu wa uadilifu wa kanisa. Angekitikisa maskini kidole hicho chenye makunyanzi usoni mwa wahubiri hao na kusema, “Mnataka kuniambia ya kwamba mnajiita watumishi wa Mungu waliopakwa mafuta, nanyi mtasimama mimbarani na kuwaacha wanawake wenu wavae kizinifu miongoni mwa wanaume, na mambo kama hayo? Mnawaacha wasichana wenu wainuke namna hiyo? Mtawaruhusu wanaume wenu kuoa mara mbili ama tatu, na wawe mashemasi makanisani? Mnataka kuniambia ya kwamba mtaushikilia utambulisho huo wenu mlio nao mkononi, na kuliweka kando Neno la Mungu?” Loo, jamani! Angekilipua kitu hicho. Naam, bwana. Utovu wa uadilifu wa kanisa, na utovu wa uadilifu wa wafuasi wake, angeulipua. Jamani! Kila mfuasi, yeye angemrarulia mbali. Kila fundisho la seminari lililobuniwa na wanadamu, angalirarua kitu hicho vipandevipande.

¹⁰⁰ Sasa, mngeweza kumpokea mtu kama huyo? La. Wasingempokea. Hakika wasingempokea. Wangemfukuza jamaa huyo kutoka mjini upesi wawezavyo. Mbona, shirika lingekutana pamoja, na kusema, “Aisee, hatuna budi kufanya jambo fulani juu ya hili. Liambi ni kusanyiko lenu wasiende

kule kusikiliza hayo.” La. La. Tusingempokea, kwa vyovyote vile, tusingempokea. Bila shaka. Wasingempokea.

¹⁰¹ Msikilizeni akilipua. Loo, ninalipenda hapa. Ninaangalia moja kwa moja kwenye yale aliyosema. Yeye alisema, “Mungu yeye yule mnayedai kumtumikia atawaangamiza.”

¹⁰² Angesema jambo lilo hilo leo hii. Sisi Wamarekani tumejifunika wenyewe sana katika mambo ya ajabu ajabu, majengo mengi sana makubwa, na idadi kubwa katika madhehebu yetu, na umaarufu huu wote mzuri, na wahudumu wa seminari waliofunzwa kutulia na kutoesema neno juu yake, kwa sababu wanaogopa watafukuzwa kanisani. Bila shaka. Angekilipua kitu hicho vipandevipande, maana ni kinyume na Neno. Hakika angekilipua. Na Mungu yeye yule tunayedai kumtumikia ata—atakitekekeza kitu hiki, moja ya siku hizi. Atakilipua vipandevipande.

¹⁰³ Amosi asingeyabadilisha maneno yake, kama angalikuwa hapa leo hii. Angedumu moja kwa moja kurudi kwenye Neno! Loo! Ati nini? Msikilizeni akiwaambia pale, “Mungu aliwapenda. Aliwaleta. Aliwafanya watu waliochaguliwa.”

¹⁰⁴ Ningetaka kumsikia kwenye kanisa la Kipentekoste wakati mmoja. Mngeliamini yeye ni Amosi, labda mngeliondoka mgongoni mwangu basi, kwa kitambo kidogo. Mnaona? Naam, yeye angewaambia. Asingewachezea. Angelilipua kwa nguvu tu kadiri alivyoweza, na kuwaambia mahali walipolipungukia Neno.

¹⁰⁵ Mungu aliyewatoa ninyi kwenye nyumba hizi za kuhifadhi maiti za kujitengenezea, zilizotengenezwa nyumbani, miaka kadhaa iliyopita! Miaka hamsini iliyopita, baba zenu na mama walitoka kwenye mifumo hii iliyokuwa imewafunga na kuingiza ulimwengu ndani yao. Ndipo Mungu akaishusha rehema Yake na kuwaita watoke, mbali na dhambi na kadhalika ambayo—ambayo ilikuwa kanisani. Na sasa mmegeuka na kurudi moja kwa moja, kama Samaria ilivyofanya. Ambapo, Mungu aliwatoa kwenye nchi hizo, nao wakageuka moja kwa moja na kufanya ushirikiano na nchi hiyo, jinsi tulivyo siku hizi, na kujaribu kushindana na makanisa hayo makubwa ya kimadhehebu. Tunajenga shule kubwa zaidi. Kitu gani? Hatuhitaji shule kubwa. Ni sawa; sina chochote cha kusema dhidi yake.

¹⁰⁶ Lakini kila wakati unapomchukua mwanzilishi ama kiongozi anayetokea katika siku zake, vema, atafanya mema katika siku zake, lakini, mara tu akiondoka, basi watajenga dhehebu juu ya kazi yake. Kisha wataliingiza kundi la maskini akina Ricky mle ndani, na akina Elvis, na, muda si muda wajua, watakipindua kitu hicho kukifanya kitosheleze matakwa yao. Halafu basi huyu *mwingine* anajitokeza na kuingiza kitu kingine, kwa sababu yeye ni mwanafunzi mkubwa wa kiakili

kutoka Harvard mahali fulani, ama kitu fulani. Ndipo jambo la kwanza, wanaanza kuingiza *hili*, na kuondoa *Hili*, na kusema *Hili* halikumaanisha *vile* na *vile*. Mmerudi moja kwa moja kwenye utaratibu ule ule wa kale tena. Naam.

¹⁰⁷ Kama Amosi angalikuwa hapa, angekilipua kitu hicho moja kwa moja akiangushe chini. Yeye hakujenga uamsho wake juu ya ni makanisa mangapi angaliweza kufanya yashirikiane naye. Kamwe asingeweza kulijenga kanisa lake juu ya madhehebu fulani wala makundi ya kanisa yenye mawazo finyu. Jambo ambalo angefanya, angejenga uamsho wake juu ya BWANA ASEMA HIVI. Mungu angemuunga mkono kama vile alivyofanya sikuzote, athibitishe kwamba ni kweli. Yeye alisema, “Kuna shida. Kuna vurugu kanisani mwenu.”

¹⁰⁸ Angesema nini leo hii? Angesema nini huku Neno hilo la Mungu likining’inia hapa nje mbele zetu? Timotheo wa Pili 3, ambapo ilisema, “Wangekuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wasiotaka kufanya suluhu, wasingizaji, wasiojizua, na wasiowapenda hao wanaojaribu kuishi vema; wenye mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake.” Unafikiri nabii angeweza kutokea jukwaani na kuukwepa unabii huo?

¹⁰⁹ Yeye atasema, “Umetimia machoni penu leo hii,” jinsi ambavyo kanisa lingekuwa la kawaida, na jinsi mambo ambayo yangefanya. Yeye ange—angewakumbusha Maneno hayo ya Mungu. Angewakumbusha yale Mungu aliyosema angefanya katika siku hii, kama Amosi angalisimama jukwaani. Si hayo tu, bali Mungu angethbitisha, kwa Amosi, yale aliyoahidi kufanya katika siku hii. Bila shaka. Angethbitisha. Alilithibitisha katika siku hiyo. Sikuzote amefanya hivyo. Bila shaka.

Tusingempokea Amosi kama angalijitokeza jukwaani.

¹¹⁰ Sasa, vipi, “Mfano huo wa utauwa,” kusimama pale juu katika—katika kwaya, na—na huku kote, kwaya kubwa zenye majoho, na—na kuimba kama Malaika; na kucheza, kesho yake usiku, kama ibilisi. Hiyo ni kweli. Mnaona? Hiyo ni kweli kabisa. Baadhi yao wanajitokeza wakiwa na majoho makubwa, marefu, yanayoonekana ya maua-maua namna hiyo, na kuonekana kama namna fulani ya Kiumbe cha kimalaika; na kusimama hapo juu na kulikana Neno, kama vile roho yeyote mchafu angefanya. “Wakiwa na mfano wa utauwa, bali wangekana nguvu zake.” Ukiendelea, kunena juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, wao, mbona, ange—angekufukuza kanisani. Mnaona? Kwa nini? Hana budi kukufukuza. Lakini watasimama katika makanisa haya na kuwaachilia wafuasi wao, katika orofa ya chini, wacheze twisti na roki.

¹¹¹ Na Y.M.C.A. zetu zinavyojiita, nashangaa kile hiyo C inachowakilisha. Ukiingia mle, ni vigumu kusikia chochote ila

Jina la Bwana li-... Kwani hilo ndilo Shirika la Vijana la Kulaani?

¹¹² Nilikaa, sio muda mrefu uliopita, katika hoteli, iliyokuwa ng'ambo ya Y.M.C.A. Na ilikuwa ni fedheha kuwaona maskini wasichana hao wadogo huko nje sakafuni, mpaka karibu saa tatu, wakijaribu kuvunja miguu yao, wakicheza hiyo twisti. Hiyo ni kweli. Nao hao wote, wafuasi wa kanisa, wanaoimba kwenye kwaya, na kufundisha shule ya Jumapili. Si kitu ila ibilisi, akiwafundisha watoto hao wadogo huko nje sakafuni, mfumo ambao umeundwa, unaoitwa dini. Bila shaka. Nabii wa kweli angekilipua kitu hicho moja kwa moja kiingie kwenye moshi wa kuzimu ambako ndiko asili yake. Bila shaka ni kweli.

¹¹³ Mnafikiri Amosi angesimama jukwaani na kuhubiri Injili, na kuangalia huko nje juu ya kundi la wanawake waliokata nywele zao na asilihukumu? Mnafikiri asingeinukuu Isaya 5, na Wakorintho wa Kwanza 14? Na, loo, hivi yeye—hivi yeye asingewamwagia hilo? Bila shaka. Angefanya hivyo. Atembee mitaani na kuwaona wanawake wamevaa nguo hizi ndogo, wakionekana kama wanaume, zinazobana sana hata ngozi iko upande wa nje, karibu hivyo; wakishuka, wakijinyonganyonga, wakitembea kwa kujifaragua, wakitembea namna hiyo, wakiliza njuga, nanyi mnafikiri mtu wa Mungu asingesimama mimbarani na kukilipua kitu hicho? Wakati, linanenwa kwa nadra sana kutoka—kutoka mimbarani. Na hiyo ni katika makanisa ya Kipentekoste, pia. Hiyo ni kweli kabisa. Haingeleta tofauti kwa Amosi. A-ha. Baadhi... Yeye angekuwa ndiye yule angesema. Asingeogopa, maana alikuwa ametiwa mafuta na Bwana. Na kama alikuwa na BWANA ASEMA HIVI, ingebidi iwe ni Neno la Bwana.

¹¹⁴ Yeye amekuja Samaria, sio kuyatazama mapambo yao, kuhesabu ni madhehebu mangapi, na idadi gani waliyokuwa nayo.

¹¹⁵ Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, inaonekana kuwa, siku hizi, kwamba kanisa zima limejengwa juu ya, jambo muhimu miongoni mwa ndugu siku hizi, wa makanisa, ni, “wingi, wingi,” mmoja akijaribu kumshinda mwenziwe. “Wingi!” Mungu hahesabu wingi. Yeye huhesabu tabia. Tabia ndiyo Mungu anayotafuta aipate, mtu fulani anayeweza kumshika kwa mikono Yake, mtu atakayesimama kimya muda mrefu vya kutosha.

¹¹⁶ Kama tulivyosema, “Maamuzi! Mwaka mzima, tulikuwa na maamuzi *kadhaa*.” Hayo ni *mawe*, “maungamo.” Nalo jiwe linafaa nini bila ya mwashi wa mawe mwenye Neno kali la Mungu, kumchonga awe mwana wa Mungu, ama binti wa Mungu, na kumweka Kanisani ambapo ndipo mahali pake? Kulingirisha mawe hakutaliyenga jengo. Inakubidi kuyakata na kuyachonga.

¹¹⁷ Tunahitaji wanaume siku hizi, wanaume waliotiwa mafuta, kama Amosi alivyokuwa, ambao wangeukatilia mbali ulimwengu kutoka kwa mwanamke huyo na kumfanya binti wa Mungu, aukatilie ulimwengu huo kutoka kwa huyo mwanamume. Bila kujali ni wadhamini wangapi waliomtupa nje, au chochote kingine, yeye angesimama juu ya BWANA ASEMA HIVI. Naam.

¹¹⁸ Tusingempokea Amosi, sidhani, namna hii. Unafikiri Amosi angefanya nini kama angetembea akaingia kwenye kanisa la Kipentekoste la leo hii, linalodai kuongozwa na Roho Mtakatifu, na halafu aone jambo lile lile katika kanisa la Kipentekoste linalodai kuongozwa na Roho Mtakatifu? Nashangaa. Sasa, tunaweza kuzungumza juu ya Wabaptisti, na Wamethodisti, na Lutheri, lakini, inapofikia kwenye mlango wetu wenyewe mchafu, basi na huo je? Tumeliondokea Neno la Mungu! Jambo fulani lilienda kombo, mahali fulani. Hiyo ni kweli kabisa. Naam. Wanakuja na kufanya mambo haya yote mbalimbali, na kudai kuongozwa na Roho, wanacheza katika Roho, wakati mwingine hata wananena kwa lugha.

¹¹⁹ Ninaamini katika kunena kwa lugha. Ninaamini katika kucheza katika Roho. Ninaamini katika kupaza sauti. Ila kuna mengi zaidi yanayoambatana na hilo. Hiyo ni kweli. Mkifanya mambo hayo yote, na kulikana Neno, basi kuna kasoro mahali fulani, mna roho mwingine. A-ha. Mungu hawaongozi watu Wake kwenye mambo kama hayo, kwa vyovyote vile. La. Hawaongozi.

¹²⁰ Nafikiri ni karibu wakati wa karamu nyingine ya kutoka, Karamu nyingine ya Chai ya Boston, kama isemwavyo. Kanisa linahitaji moja. Linahitaji kusafishwa vizuri kwelikweli.

¹²¹ Wakati, Joan wa Arc, katika siku zilizopita, kanisa Katoliki lilikosa kujua ya kwamba yeye alikuwa ni mtakatifu alipokuwa hai, kwa sababu aliona maono, angeweza kufasiri ndoto, mwanamke aliyejazwa na Roho. Naye Mungu alimtumia maskini msichana huyo. Nao walidhani alikuwa ni mchawi. Ndipo wakamchoma moto kwenye nguzo, kama mchawi. Mnajua jambo hilo. Makasisi wa Kikatoliki walifanya hivyo wenyewe. Mamia ya miaka ilipita, ndipo wakakuta kwamba alikuwa ni mtakatifu. Basi, walipokuwa wakienda kumfanya mtakatifu, iliwabidi kufanya vitubio. Kwa hiyo wakachimbua mwili wa makasisi hao na kuitupa mtoni, kufanya vitubio. Mnaona, lilipita moja kwa moja karibu nao wakashindwa kuliona. Walifanya karibu jambo lilo hilo na Mtakatifu Patrick na hao wengine wote.

¹²² Si ajabu Yesu alisema, “Mnayapamba na kuyapaka chokaa makaburi ya manabii, nanyi ndio mliowaweka mle ndani.” Hiyo ni kweli. Tunachohitaji leo hii ni Amosi fulani atakayelirejesha Neno la Bwana kwetu. Hakika tunamhitaji.

¹²³ Sasa, madai yetu na kadhalika hayamaanishi kitu isipokuwa Roho wa Mungu yupo kuyaunga mkono madai yetu. Iwapo maisha yetu hayalingani na madai yetu, basi kuna kasoro fulani.

¹²⁴ Joan wa Arc aliongoza Ufaransa katika mapinduzi. Walihitaji mwanamapinduzi. Hivyo ndivyo walivyofanya hasa. Walihitaji mwanamapinduzi, naye akayaongoza. Lakini baada ya hayo mapinduzi, mahali kosa lilipotokea, walihitaji mapinduzi pinzani kuyanyosha—kuyanyosha yale waliyokuwa wakiasi.

¹²⁵ Ninasema kanisa la Kipentekoste ndicho kitu nijuacho kilicho karibu zaidi na Biblia leo hii. Kama sivyo, ningekuwa katika jingine. Hiyo ni kweli. Nisingekuwa nikisimama hapa nikipoteza wakati wangu, nikizungumza na Wapentekoste, kama sikuwazia kulikuwako na matumaini. Kweli. Pentekoste ni ya kweli. Lakini tunapohitaji Pentekoste ije pamoja na kuvunjilia mbali mapokeo yetu, basi tunahitaji mapinduzi pinzani. Tunahitaji kuja kupinzani; nina ninii...sio dai la Kipentekoste, bali kuja kwa utakaso wa Kipentekoste.

¹²⁶ Mungu ni mtakatifu. Wale wanaoishi Kwake hawana budi kuishi watakatifu. Yeye ni Mungu mtakatifu. Biblia ilisema, “Pasipo na utakatifu, hapana mtu atakayemwona Bwana.” Hiyo ni kweli. Uzima Wake ni mtakatifu. Basi kama Uzima Wake uko ndani yako, unakufanya mtakatifu. Pasipo na huo, humwoni Bwana. Basi angalia mahali linakoelekea.

¹²⁷ Sisi ni kitu kama Israeli ilivyokuwa katika siku hizo, hata hivyo. Israeli iliwazia, kwa sababu kwamba walikuwa wakifanikiwa, kila kitu kilikuwa kikienda vema. Walikuwa na ushirikiano, katika siku zao, pamoja na miji mingine. Nao walikuwa na ushirikiano. Serikali ilikuwa na ushirikiano na wahudumu, pamoja na makuhani, pamoja na manabii. Nao walidhani hili lilikuwa ni sawa. Nao walidhani hilo lilikuwa tu linampendeza Bwana. Bali walikuwa na maskini jamaa aliyeinuka na kuwarudisha tena. Hiyo ni kweli.

¹²⁸ Kwa sababu tu walifanikiwa, hapo ndipo tunapofanya kosa. Mafanikio sio ishara ya baraka za kiroho. Hiyo ni kweli. Si hata kidogo. Mafanikio, wakati mwingine, ni kizuizi.

¹²⁹ Mnakumbuka kile Bwana alichosema kuhusu Israeli? “Ulipokuwa mdogo, ulipokuwa huna kitu, wakati ulipolala katika damu yako mwenyewe kondeni, hakuna mtu wa kukusafisha, nilikuchukua. Ndipo ukanitumikia. Lakini ulipokuwa mtu mzima vya kutosha hata ukawazia ulikuwa sawa na umejifanya salama, basi uliniacha.” Daima wamefanya hivyo.

¹³⁰ Uzia, kama nilivyomzungumzia kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara hivi majuzi asubuhi, yeye alikuwa mtu mashuhuri. Alimshikilia Bwana. Lakini siku moja baada ya Mungu kumuimarisha...Naye alikuwa ni mfano mkubwa kwa

Isaya nabii. Lakini baada ya kuimarika, na kujijenga, mataifa yalianza kumwogopa. Alijenga kuta zake na kuanza kupata vitu vya madoido. Akashikwa na kiburi. Akaanza kuangalia jinsi alivyokuwa mkuu. Ndipo basi akajaribu kupachukua mahali pa mhubiri. Naye Mungu akampiga kwa ukoma, na akafa mwenye ukoma. Mnaona? Kamwe hatutaki kujiinua, miyoyoni mwetu.

¹³¹ Na wakati mwingine, tunapoona madhehebu yetu yakifanikiwa, tunaanza kusema, “Sisi ndio kundi kubwa. Si ndio kundi kubwa kuliko yote ya Kipentekoste lililopo. Tuna wengi kuliko hao wengine.” Ama, “Huwezi kwenda Mbinguni isipokuwa uwe ni wa kundi letu,” ama kitu fulani. Unapokuwa hivyo, umejitenga mwenyewe na Neno la Bwana. Kweli. Kumbukeni, blanketi ni pana vya kutosha kumfikia ndugu yako. Hiyo ni kweli kabisa. Mwingize ndani.

¹³² Loo, jinsi tunavyohitaji, leo hii, wito wa kurejea kwenye Neno la Bwana. Angalieni, siku hizi. Nalo taifa letu linahitaji wito wa kurejea.

¹³³ Nitazungumzia, moja ya siku hizi usiku, nikiweza, ninataka...Ninalo shtaka. Inanipasa kungojea mpaka niwakusanye wahubiri wote pamoja. Naam. Ninataka kukishtakia kizazi hiki Damu ya Yesu Kristo, na kuwathibitishieni. Mnaona? Sasa, huenda ikanibidi, kuenda nje mahali fulani kufanyia hilo. Lakini tutaninii, tutaona kama tunaweza kuwa na kiamshakinywa asubuhi moja, kwa ajili ya wahudumu pekee. Na mimi—mimi nataka, Bwana akinisaidia, kuonyesha mahali tulipo hasa—mahali tunapoelekea, njia mbaya. Hatuna budi kurudi. Hakuna njia nyingine ila kurudi. Kweli.

¹³⁴ Liangalieni taifa letu siku hizi. Angalieni yale tunayotaribu kufanya, jambo lile lile lililotendeka katika wakati wa giza, kuunganisha kanisa na taifa pamoja.

¹³⁵ Angalieni huko kuungana, muungano, ama Ba—Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Makanisa yote yanaingia kwenye hili Baraza la Makanisa Ulimwenguni, nao wanafikiri huu ni umoja wa Mungu. Kwa sababu, makanisa yote, Muungano wa Ndugu, watu wa makanisa ya kimsingi, wanaingia kwenye shirika hili moja kubwa. Hiyo ni kwa sababu ya kutolifahamu Neno la Mungu. Nabii alisema ya kwamba jambo hilo lingetukia, “Wangefanya sanamu ya mnyama, nayo ingekuwa na uwezo wa kunena.”

¹³⁶ Loo, mnafikiri Amosi angeweza kusimama mimbarani usiku wa leo hapa chini, kama alikuwa katika Phoenix, na kushindwa kulikemea jambo hilo? Haingekuwa kwamba angekuwa anatupinga, ndugu, bali angekuwa akiupinga mfumo unaotuongosha kwenye Neno. Hivyo ndivyo yeye angefanya. “Watu hao wanawezaje kutembea pamoja?” Biblia ilisema hapa,

hapa ndani, Amosi. Bwana alisema, “Waambie hao watu, ‘Watu wawili wanawezaje kutembea pamoja, wasipopatana?’”

¹³⁷ Sasa, tutayachukua je makundi yetu ya Kipentekoste na kuingia katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni, wakati nusu yao mle ndani, zaidi ya nusu, asilimia themanini na tano ama tisini na tano, hata wanakanusha kuzaliwa na bikira? Wanakana. Nadhani, asilimia tisini na tisa yao wanakana, wanakana uponyaji wa Kiungu. Wanazikana kanuni za Biblia. Wanakana kunena kwa lugha. Kundi la Kipentekoste tu ndilo linalokuchukua huko. Basi tutajiunganishaje pamoja nao katika umoja? Tutakuwaje mmoja pamoja nao? Tutatembeaje pamoja nao pasipo kupatana nao? Mtafanyaje jambo hilo? Itawalazimu kukanusha ile imani kuu ya kiinjilisti mliyo nayo, kanuni za kimsingi za Biblia, mpate kutembea pamoja nao.

¹³⁸ Nawaambia, Mungu humwita mtu binafsi. Yeye anakuita, kama mtu binafsi, kudumu na Neno Lake na kudumu na Yeye.

¹³⁹ Mungu angewezaje kutembea pamoja nao, wakati kanuni zao wenyewe za imani, zilizobuniwa na hekima yao wenyewe ya kilimwengu, zinalikana Neno Lake? Wakati kanuni ya imani inapolikubali fundisho la kundi la watu, pamoja, na kukana Neno kuwa ni kweli, basi mnamwondosha Mungu kweni. Mungu ni mtakatifu. Naye Mungu, Biblia inasema, Yeye huliangalia Neno Lake, apate kulithibitisha. Basi anawezaje Yeye kulithibitisha Neno, wakati Neno halipo? Hiyo ndiyo sababu tunao wafuasi badala ya watoto. Hiyo ni kusema, tuna kanuni ya imani. Na kila mtu anaweza . . .

¹⁴⁰ Ulimwengu unatafuta mtu mkuu. Wanafanya kazi kwa ajili ya . . . Wanatafuta kitu ambacho kinaweza kuwaacha washikilie maungamo yao ya Ukristo na kuishi vyovyote watakavyo. Wanawake wanataka kutenda kama Hollywood na bado washikilie ya kwamba wana Roho Mtakatifu. Wahubiri wanataka kujenga kanisa lililo kubwa kuliko yote na kufanya mambo haya yote, na kuwa na mashemasi waliooa mara nyingi. Na—nao wanaweza kufanya mambo haya madogo na kuvaa nguo *hizi*, wanauita ukombozi wa wanawake.

¹⁴¹ Unafikiri Amosi angevumilia jambo hilo? La. Asingeweza hashi. Unafikiri Amosi angesimama kimya, na kukutana na uongozi msonge na maaskofu huko juu, na kusema, “Ndugu, nafikiri mmefanya jambo zuri sana.”

¹⁴² Angesema, “Enyi kundi la wahaini! Enyi waigaji! Enyi wenye kuikana Imani!” Angesema jambo lile lile ambalo Mikaya alisema, ile siku mbele ya hao manabii mia nne wa Kiebrania wenye kujifaharisha.

¹⁴³ Walisema, “Katika wingi, umati ndio, basi pana usalama.” Inategemea ni wapi unakotaka kulitumia Andiko hilo.

¹⁴⁴ Ninaweza kusema, “Yuda alienda akajinyonga; nawe unaenda unafanya jambo lilo hilo.” Halitumiki hapo.

¹⁴⁵ Wala halitumiki, kwamba, “Katika wingi wa ushauri kuna usalama.” Kanisa Katoliki limewashinda ninyi nyote basi.

¹⁴⁶ Katika Neno la Mungu kuna usalama. Biblia ilisema, “Jina la Bwana ni ngome imara. Wenye haki huikimbilia wakawa salama.” Na hapo ndipo mahali pekee pa salama nipajuapo. Manabii daima waliamini hilo. Wakati Ibrahimu alipokufa, wakati... Wakati Ayubu alipokufa, yeye alijilaza kwenye nchi ya ahadi, kaburi lake.

¹⁴⁷ Wakati Ibrahimu alipokufa, alinunua kipande cha ardhi moja kwa moja karibu na mahali papo hapo, karibu na Ayubu. Alifanya nini? Alimwalia nabii huyo. Alijua huyo alikuwa ni mtu wa Mungu, naye alisema, “Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho, atasimama juu ya nchi. Ingawa baada ya mabuu ya ngozi kuuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu.” Naam. Naye Ibrahimu alijua hilo. Akamzika Sara hapo. Alinunua kipande cha ardhi, na kumzika... Yeye, mwenyewe, alizikwa hapo.

¹⁴⁸ Isaka, alipokufa, alirudishwa akazikwa hapo. Isaka alimzaa Yakobo.

¹⁴⁹ Ndipo Yakobo akafa huko chini kabisa katika Misri. Lakini kabla hajafa, yeye alimwita nabii mwanawe, Yusufu. Naye alijua ya kwamba alikuwa ni nabii, mtu wa kiroho, alifasiri ndoto, na kuona maono, yaliyokuwa sahihi kabisa kila wakati. Akasema, “Njoo hapa, Yusufu, mwanangu nabii. Weka mkono wako juu ya nyonga hii ambapo mwenyezi Mungu alinigusa miaka kadhaa iliyopita, na kulibadilisha jina langu kutoka ‘mtwaa mahali pa mwingine’ nikawa ‘mtawala pamoja na Mungu.’ Weka mikono yako hapa juu na kuapa kwa Mungu ya kwamba hutanizika hapa chini katika Misri.” Kwa nini? Kwa nini? Ileta tofauti gani?

¹⁵⁰ Hivyo ndivyo wanavyosema siku hizi, “Inaleta tofauti gani?” Tunalichukua kundi la watu, tunawafanya wajiunge na kanisa, na kuondoka mitaani. Wakati mwingine unamfanya maradufu mtoto wa kuzimu kuliko alivyokuwa huko nje mtaani. Hiyo ni kweli. Kweli inaleta tofauti.

¹⁵¹ Yusufu, alipokufa, alitaja, akasema, “Siku moja Bwana Mungu atawazuru.” Yeye alikuwa ni nabii. Akasema, “Bwana Mungu atawazuru. Na msiiache mifupa yangu huku chini, bali ichukueni muipeleke kwenye nchi ya ahadi.” Kwa nini? Yeye alijua ya kwamba Malimbuko ya ufufuo yangetokea kwenye nchi ya ahadi. Hiyo ni kweli kabisa.

¹⁵² Yesu, wakati alipokufa, na kufufuka kwenye asubuhi ya Pasaka, Biblia ilisema, ya kwamba, “Wengi wa watakatifu waliolala katika mavumbi walifufuka, wakatoka makaburini na wakawatokea wengi.” Alikuwa ni nani? Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Yusufu. Kwa nini? Walikuwa mahali pazuri.

¹⁵³ Hiyo ndiyo sababu ninasema kweli inaleta tofauti. Msinzike tu hapa nje katika Methodisti fulani, Baptisti, wala kanisa fulani

lingine. Nizike katika Yesu, “Kwa kuwa hao walio katika Kristo Mungu atakuja pamoja nao hapo Yeye ajapo.” Na kweli inaleta tofauti. Hakika, inaleta.

Usiache mtu fulani akwambie, “Kwa sababu unajiunga na kanisa.”

¹⁵⁴ Amosi asingevumilia hilo. Yeye angesema, “Mungu yeye yule mnayesema kwamba mnamtumikia. . .”

¹⁵⁵ Ningesema jambo hili katika Jina la Bwana: Mungu yeye yule ambaye taifa hili linadhaniwa linamwakilisha ataliangamiza taifa hili. Atayaangamiza makanisa haya. Mungu wa Mbinguni ataishusha ghadhabu Yake katika hukumu na kuyaangamiza makanisa haya, yanayojiita makanisa. Kumbukeni, ninyi lishikeni neno langu.

¹⁵⁶ Hakuna mtu anayeweza kujiunga na Kanisa. Unajiunga na chama. Hujiungi na Kanisa. Unazaliwa katika Kanisa. Unaona? Unajiunga na chama cha Kimethodisti, chama cha Kibaptisti, chama cha Kikatoliki, chama cha Kipentekoste. Bali unazaliwa katika Kanisa la Mungu aliye hai; na hilo ndilo analolijia, Kanisa hilo. Kwa hiyo, tuna vyama, sio Makanisa. Chochote kinaweza kukusanyika kwenye chama hicho, wanafiki na kila kitu kingine. Lakini nitawafahamisha hili sasa hivi, kulingana na Neno, hakuna mnafiki hata mmoja katika Kanisa la Mungu aliye hai. Hakuna kitu Mle ila watakatifu.

¹⁵⁷ Sasa, uanachama unaweza kukuingiza ndani. Nawe unafikiri—unafikiri Amosi asingalilipua hilo? Angekitikisa kitu hicho hata kwenye msingi wake. Hakika angekitikisa.

¹⁵⁸ Tazama. Wakati Israeli walipokuwa safarini, wakielekea kwenye nchi ya ahadi, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, Nguzo ya Moto iliwatangulia, Mwamba uliopigwa ukawafuata.

¹⁵⁹ Ndipo Moabu akajitokeza, ambaye alikuwa ni ndugu. Kumbukeni, yeye alikuwa ni sehemu ya Israeli, pia. Alikuwa sehemu, kutoka kwenye ukoo huo wa Kiyahudi, maana alikuwa ni mtoto wa Lutu kwa binti yake. Ilimzaa Moabu.

¹⁶⁰ Pia mtazameni Balaamu, yule kuhani, alijitokeza huko na kufanya madhabahu, akatoa dhabihu za namna ile ile, wa kimsingi tu alivyoweza kuwa. Mnaona? Naye alikuwa pamoja na watu maarufu. Alikuwa na mfalme. Alikuwa na watu wote mashuhuri, watawala na matowashi, wamesimama pamoja naye.

¹⁶¹ Ila palikuwapo na Mmoja aliyesimama pamoja na Musa ambaye yeye hakumwona. Huyu Ndiye aliyesimama pamoja na Amosi. Huyu Ndiye atakayesimama na kila mtu aliyepo hapa, usiku wa leo, atakayemtetea Mungu pamoja na haki. Haidhuru ni watawala wangapi, watawala wakuu waliopo, halina uhusiano wowote nalo. Kamwe hawataweza kulaani kile Mungu amebariki. Kwa nini? Ni Mbegu iliyo hai. Ni Neno la

Mungu. Litakua lifikie ukamilifu Wake. Loo, ishara za Mungu aliye hai kambini! Hiyo ni, ilionekana kana kwamba Israeli walikuwa wamefanya makosa kule chini. Bali wanashindwa kuona Mwamba ule uliopigwa, na ule Upatanisho uliofanywa kwa ajili ya Israeli. Pia kulikuwako na shangwe za Mfalme kambini. Mungu alikuwa pamoja nao. Kwa nini? Yeye alikuwa akiwaponya wagonjwa, na kufanya miujiza mikubwa, na ishara na maajabu, na Nguzo ya Moto ikining'inia juu yao. Musa alikuwa akiifuata ile Nguzo ya Moto. Wana wa Israeli walikuwa wakimfuata Musa. Nao walikuwa njiani mwao wakielekea kwenye nchi ya ahadi, wala hakuna kitakachowazuia. Amina.

¹⁶² Loo, hivi si lingerudiwa kwa urahisi leo hii, kama Mungu angeweza kumpata mtu fulani mkononi Mwake, chini ya udhibiti Wake? Hiyo Nguzo ya Moto ingali hai. Yeye angali ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Neno lingali hai.

¹⁶³ Mungu, tutumie Amosi ambaye... ambaye ataitetea Kweli na haki, akayatikise mambo haya.

¹⁶⁴ Unasema, "Tungeweza... Unafikiri angepata matokeo ya namna gani?"

¹⁶⁵ Vema, angepata matokeo, hata angewaita hao wote ambao Mungu alikuwa amewachagua tangu mwanzo wapate kuitwa. Hao ndio angewapata. "Wote alionipa Baba watakuja." Naam.

¹⁶⁶ Mikaya alikuwa mbele ya Ahabu, naye Ahabu alimchukia. Kundi lote la wahudumu lilimchukia. Na hao wote walikuwa wamevuviwa, pia, bali uvuvio wao haukuambatana na Neno. Nadhani, labda, Amosi alikikemea kitu hicho hicho.

¹⁶⁷ Wakati makuhani walipotembea mtaani, walisema, "Sasa, ngoja kidogo. Wapi—wapi... Nionyeshe hati zako za utambulisho. Ulitoka kwenye shule gani? Ulitoka kwenye ukoo gani? Hivi wewe ni... Ni nani aliyekufanya kuhani?"

Angesema, "Mungu alinifanya kuhani."

"Umetokea shule gani?"

¹⁶⁸ "Yehova Mungu. Nina BWANA ASEMA HIVI." Watamsikiliza? La hashu. Hawakutaka kumsikia jamaa huyo. La hashu. Hawakutaka...

¹⁶⁹ Na, hata hivyo, hao watu huenda walisema, "Mimi nimevuviwa. Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa kuu la Mafarisayo hapa. Angalia jinsi Mungu ametubariki. Tumeweka madhabahu ya dhahabu. Tumejenga mahekalu. Tumefanya mambo haya yote. Na, loo, matoleo yetu ya umishenari ni makubwa kuliko lolote la makanisa hayo mengine kote katika Yuda. Vema, tunafanya mambo haya yote *hapa*. Watu wetu ni walipa zaka wakubwa sana, na yote hayo." Lakini hata hivyo Mikaya ama...

¹⁷⁰ Amosi alisimama pale na kusema, "Mungu yule mnayedai kwamba mnamtumikia atawaangamiza." Na ilitukia hivyo.

¹⁷¹ Sasa, siihukumu mipango ya umishenari. Siyahukumu makanisa makubwa. Lakini, shida yake ni kwamba, watu huyaelekeza macho yao kwa hayo, na juu ya . . . mbali na Neno. Ndipo, hatimaye, linakuondoa moja kwa moja likakuingiza kwenye kitu hicho, ndipo unajikuta ukiteleza. Rudi moja kwa moja kwenye Neno. Usiliondokee. Loo, jinsi tunavyohitaji kilio, kutoka nyikani leo. Bila shaka ni kweli sasa. Bila shaka.

¹⁷² Sababu zingine, watu wanatoa hoja. Wanataka kutoa hoja. Hilo ndilo jambo la kwanza lililoninii . . . Hilo ndilo lililopoteza ushirika wa jamii ya binadamu, ni wakati Shetani alipoingiza mpango wa kutoa hoja dhidi ya Neno kuwa ni kweli. Nalo linasikika lenye hoja nzuri sana.

¹⁷³ Hebu tumchukue tu Shetani, kile huenda alimwambia Hawa, wakati Mungu alipowazingira kwa Neno Lake.

¹⁷⁴ Hicho ndicho kitu pekee ambacho Mungu alipata kuwapa watu Wake kuwakinga na adui, kilikuwa ni Neno. Kamwe hakutupatia kanuni ya imani. Hakutupatia kitu ila Neno Lake. Hilo tu. Naye Mungu hana kikomo, yuna nguvu zote, habadiliki. Hawezi kubadilika. Mpango Wake wa kwanza ni mkamilifu. Kamwe haimbidi kuubadilisha.

¹⁷⁵ Uamuzi Wake wa kwanza, wakati mwanadamu alipotenda dhambi na kuvuka shimo hilo kubwa kati yake na Mungu, pasipo kujiachia njia ya kurudi, Mungu, mwingi wa rehema na neema, alikubali kibadala. Mungu aliyejaa rehema na neema ndiye tu angeweza kufanya jambo kama hilo. Alikubali kibadala, na kibadala hicho kilikuwa ni damu. Hapo ndipo mahali pekee ambapo mwanadamu angeweza kuingia katika ushirika pamoja na Mungu tena, ni chini ya damu iliyomwagika. Na hapajakuwapo na wakati wowote ambapo mwanadamu angeweza kufanya ushirika pamoja na Mungu, ni kwa hiyo damu pekee. Na ni kweli kabisa, mahali anapofanya ushirika na Mungu.

¹⁷⁶ Sasa, Hawa aliachilia mambo. Hawa alianza kutoa hoja. Shetani alisema hivi, “Sasa, wewe ni . . . Hujui. Hujasomeshwa bado. Mimi ni profesa wa ile seminari kule nje.” Yake mwenyewe. “Na, nakwambia, tumesoma mambo fulani huko nje. Tulisoma kwamba Mungu ni mwema sana! Tulisoma katika seminari yetu ya kwamba Mungu ni mwema sana! Hakutarajii kufanya yote aliyoandika mle. Hatarajii hilo.”

“Naam, lakini,” mwanamke akasema, “Bwana Mungu alisema.”

¹⁷⁷ Sasa, yeye angalifanya mhubiri mzuri, kama angalidumu kwenye Hilo. Hiyo ndiyo sababu amehukumiwa asiwe mhubiri leo hii. Mnaona? Mwekeni mbali nalo. Amosi angesema nini kuhusu hilo? Laiti ningaliweza kumsikia kwa kama dakika tano, na kuurekodi ujumbe wake. Ningeuweka moja kwa moja kwenye kanda, nifanye ulimwengu mzima kuusikia. A-ha.

Halafu ningeweza kunyamaza kuuhusu, tangu wakati huo na kuendelea. Tazameni. Naam, bwana, yeye angelilihukumu.

¹⁷⁸ Pia angalia yale aliyosema. Sasa, Shetani alisema . . . Sasa, yeye asingeweza kufanya hivyo na Hawa, mwajua . . .

¹⁷⁹ Asingeweza kufanya hivyo na Adamu, bali alilifanya na Hawa. Kwa hiyo akamwambia Hawa, sasa, “Sasa unajua *hili*.” Akasema, “Unajua, hakika Mungu ni mwema sana asingeweza kukudhuru. Mungu . . . Hakika hutakufa. Unajua Yeye ni Mungu mwema.”

¹⁸⁰ Tunasikia mengi sana kuhusu hayo siku hizi. Yeye ni Mungu mwema. Lakini, ili aweze kuwa mwema, hana budi kuwa mwenye haki, pia. Hilo ndilo linalomfanya mwema. Yeye si asiye na msimamo. Yeye ni Mungu.

¹⁸¹ Na sasa, “Mungu ni mwema sana asingeweza kukufanyia jambo hilo.” Naye akaanza, kasema, “Mbona, utakuwa mwenye hekima. Utakuwa na elimu. Utakuwa mwerevu na mwenye hekima. Uta—utajua mambo usiyojua sasa.” Mnaona?

¹⁸² Ilimbidi tu kujua jambo moja, hilo lilikuwa ni Neno. Haitubidi kuwa na Shahada ya Sanaa, na Ph.D., na LL.D., na mambo haya yote mengine. Lijue tu Neno la Mungu. Mtoto aliye rahisi kuliko wote, anayeweza kusoma, anaweza kulijua, kujua.

¹⁸³ Lakini, hoja, basi walipata nini? Walipata kitu gani? Papo hapo walivurugika. Naye Shetani alijua aliishinda jamii ya binadamu papo hapo. Na hapo ndipo amewashindia tangu wakati huo.

¹⁸⁴ Hiyo ndiyo sababu Amosi alikuja. Kwa sababu, umaarufu na maoni yanayopendwa na wengi, pamoja na rais ama mfalme mzuri, mkuu, aliyekuwa amelea ufanisi. Watu wataua haki zao kwa mlo wa maharage, kama vile Esau. Sijaribu kuudhi, bali ninajaribu kusema ukweli.

¹⁸⁵ Ninyi Wanademokrasia mliuza haki zenu za mzaliwa wa kwanza muda si mrefu uliopita. Hiyo ni kweli. Na mimi si Mripablikani. Mimi ni Mkristo. Lakini, ndugu, ni fedheha jinsi gani! Na iliwabidi kuchukua mashine iliyofanyiwa ujanja kupigia kura namna hiyo. Lakini hilo ndilo Marekani ililotaka. Walilipata. Yeye kwa kawaida hukupa unalotaka.

¹⁸⁶ Mungu, nipe Neno Lako. Hilo ndilo ninalotaka. “Jalia nilifiche Neno Lako moyoni mwangu, Bwana, nisije nikafanya dhambi dhidi Yako.”

¹⁸⁷ Loo, wengine huhoji. Lakini, mnaona, Amosi asingeweza kuhoji, kwa sababu yeye alikuwa ni nabii. Neno lilimjia. La.

¹⁸⁸ Kama vile Neno leo hii, huna budi kulifasiri, umwache Roho Mtakatifu alifasiri kwa kulithibitisha maishani mwako.

¹⁸⁹ Hayo ndiyo yaliyosemwa, yale, mwajua, Yeremia aliyomwambia na—nabii Hanania. Yeye alisema, “Nabii huyo

anaponena, na yale asemayo yadhihirishwe, basi manabii walijua yeye alikuwa sahihi.”

¹⁹⁰ Kama Amosi angalikuwa hapa, unafikiri angalifanya nini? Ange—angedumu na Neno. Hivyo ndivyo angefanya. Mnajua nini? Angetwambia ya kwamba tumefundishwa tukaondolewa kwenye msingi wa Neno asili la Mungu. Angetwambia ya kwamba tuko mbali sana na Kanisa la kwanza la kipentekoste. Hivyo ndivyo angetwambia sisi Wapentekoste. Kasema, “Sasa, walikuwa na karibu miaka hamsini ya kujiandaa, wala hamjafikia mahali hapo bado.” Loo, angemwambiaje mtu wa kimadhehebu? Vema, loo, kama hangetoa hilo, kama hangeyararua hayo makanisa, kwa ajili ya utovu wao wa uadilifu, kwa kuzikubali kanuni za imani, kujiunga na kanisa badala ya kuzaliwa ndani yake!

¹⁹¹ Vema, kama umezaliwa ndani yake, ndugu, dada, unatenda tofauti. U—unadumu na Neno. Kama Roho Mtakatifu yuko ndani yako, Yeye hula tu Neno. Yesu alisema, “Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno,” sio sehemu ya Neno, “bali kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.”

¹⁹² Yeye, akiwa ni nabii, angeweza kuona jambo hili ndani yetu. La . . . Amosi alikuwa ni nabii.

¹⁹³ Sasa, nitafunga, katika dakika moja, bali ninataka kutoa matamshi haya yashikilie kama nikiweza. Nitalisema, naye Roho Mtakatifu hana budi kulifanya lishike. Ninataka kuwaulizeni jambo fulani.

¹⁹⁴ Kama Amosi alikuja hapa usiku wa leo na kusimama kwenye jukwaa hili, kama alitembea juu chini katika mitaa ya Phoenix, angeona ndani yetu leo, katika mambo yetu ya kitaifa, katika ulimwengu wetu wa kanisa, angeona jambo lile lile aliloona huko Samaria: wamezama kabisa katika utovu wa uadilifu, mbali na Neno la Mungu. Angeona kundi la kidini sana. Walikuwa, kila mmoja wao, Israeli. Lakini angeona u—utovu wa uadilifu, ufisadi. Angeona—angeona uozo wa jamii na utovu wa maadili miongoni mwa watu. Angeona uozo wa maadili miongoni, juu ya taifa. Angeona uozo wa maadili kutoka kwa Neno. Angeona uzinzi kanisani. Simaanishi . . . Naam, zote mbili; wa kimwili, na angeona uzinzi wa kiroho. Jinsi ambavyo wangekuwa wakichukua kanuni za imani za wanadamu hapa nje, kama kanuni za imani za mwanadamu, na kuzikubali badala ya Neno, hiyo ni kufanya uzinzi wa kiroho dhidi ya Mungu. Ufunuo 17 inasema hivyo, ya kwamba wao, kahaba huyu, alitenda dhambi, kwa sababu, “Kwa machukizo yake aliifanya nchi kunywa mvinyo wa ghadhabu yake.” Naam. Tunaona kwa jumla ingekuwa tofauti. Yeye angeuona, uozo wa maadili.

¹⁹⁵ Amosi kamwe hakuilaumu serikali, hata hivyo. Sikilizeni. Amosi kamwe hakuilaumu serikali, katika Maandiko yake yote.

Bali aliwalaumu watu kwa kuichagua serikali ya aina hiyo. Loo, ningenii. . .

¹⁹⁶ Mmechoka? [Kusanyiko linasema, “La.”—Mh.] Vema, tulieni tu kwa dakika moja. Mnaona?

¹⁹⁷ Msiilaumu serikali yenu. Serikali haiwezi kujenga nyumba juu ya mwamba ambapo watu wanapigia kura mchanga. Watu wanaitaka.

¹⁹⁸ Na mara nyingi mimi husema mambo mimbarani, wakati nikijua ndugu zangu wameketi huko nje, wahudumu, watu wazuri. Mimi huzungumza nao, ninawaweka kwenye kona. Na ni jukumu langu, nikijua mambo haya, kuwaambia ndugu zangu. Nami huzungumza nao. Wanasema, “Ndugu Branham, tunajua uko sahihi, bali kanisa langu litanitoroka.” Mnaona? Mnaona? Ni yale mnayotaka. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Mnaona? Hamwezi. Ni watu.

¹⁹⁹ Sasa, kama mnafikiri ningeanza jengo hapa chini mtaani na kuwauzia, kina mama siku hizi, viatu vile vya mtindo wa kale, vilivyopanda juu mguuni, vya kamba? Huenda vina ngozi nyingi kuliko—kuliko duka zima lililojaa lilizo nazo siku hizi, jozi moja. Lakini kama nikiviuza kwa senti hamsini kwa jozi, ningekufa kwa njaa. Kwa nini? Hamvitaki.

²⁰⁰ Kama ningaliuza zile sketi za mtindo wa kale, za Mama Hubbard, kwa wanawake leo, unafikiri wangezinunua? La hasha. Wanataka kitu ambacho wangepewa kujimiminia ndani yake, kinachoonekana kama ngozi juu ya soseji. Wao—wanataka viwabane kabisa. Wakitembea mtaani, kama digrii nne ama tano mbalimbali, wamesukumwa ndani, wakasukumwa nje, na wameegemea nyuma juu ya jozi ya visigino, kichwa chao kimetokeza nje. Hilo ni, simaanishi hilo kwa mzaha. Hapa si mahali pa mzaha. Lakini hiyo ni kweli. Sina elimu nzuri. Hivyo ndivyo tu ninavyoweza kulielezea neno langu, kujua, mpate kujua ninalomaanisha. Mnaona? Sasa, ni kweli. Wasingezinunua hizo nguo.

²⁰¹ Hivi majuzi usiku jukwaani, maskini mwanamke wa Kihindi alipanda hapa juu. Nilitaka kumsalimia kwa mkono. Huko kwenye kanisa la Ndugu Groomer, ama popote pale. Alikuwa amevaa gauni kama alilovaa mama yangu. Nikawaza, “Vema, nautakia heri moyo wako, mama.” Ndipo Bwana akamponya papo hapo, kabla hata hajanifikia. Yeye. . . Mnaona? Niliwaza, “A—a—afadhali tu nitulie.” Mnaona? “Kungojea tu mpaka nafasi ije, wakati mwingine.” Mnaona? Na hiyo hapo.

²⁰² Vema, usingeweza kuyauza magauni hayo. Huenda ukayauza kwa Mhindi, na sio wengi sana wa hao. Wanakuwa wapotovu tu kama hao wengine. Mna vipindi vingi mno vya televisheni. Nao watoto wenu wakitoka nje, na baadhi ya hawa walimu wazungu wa kisasa, wakiingia, na upuuzi huu mwingine wote.

Mngekuwa afadhali, mngalikuwa huko nje kama Sitting Bull na hao wengine walivyokuwa, zamani za kale.

²⁰³ Huko Afrika, tulipokuwa na watu weusi huko, wanafanya nini? Wanaenda huko, hao wamishenari, ni kusoma, kuandika, na hisabati. Wakati yeye... Mbona, hao, wanajua zaidi juu ya uadilifu, katika makabila yao, kuliko mngaliweza, Ukristo ungaliweza kuwaletea. Hiyo ni kweli. Kama yeyote wa hao wanawake huko nje, kama yuko kwenye kabila la Zulu, kama akingojea kufikia umri fulani kuolewa, na bado, mtu fulani hajamchukua kama mke, hana budi kuondoka huko. Yeye si wa kabila hilo tena. La, bwana. Na anapoolewa, yeye anachunguzwa ubikira. Na kama akipatikana na hatia, hana budi kumsema mwanamume aliyefanya hivyo, ndipo wote wawili wanauawa, pamoja.

²⁰⁴ Kungekuwako na mauaji mengi huku kama tungalikuwa na mpangilio wa namna hiyo. Sivyo? Hiyo ni kweli. Hawangekuwa na wazishi wa kutosha kuwazika wanaume na wanawake. Bila shaka. "Lakini umekufa, kwa vyovyote vile, wala hujui." Kwa hiyo hiyo ndiyo shida yake. Mnaona? Lakini sasa, mengi sana, hiyo ni kweli.

²⁰⁵ Basi unafanya nini? Wanawapeleka kule na kuwafundisha shule. Kisha unawapata mtaani. Wanazo dhambi zao wenyewe za kikabila, walizokuwa nazo; ndipo wanaingia, wanazichukua dhambi za wazungu; halafu hao ni mara kumi mwana wa kuzimu kuliko walivyokuwa mwanzoni. Kitu pekee wanachohitaji ni Kristo, kukaa mahali walipo. Kweli.

²⁰⁶ Hivyo ndivyo ilivyo kwa Wahindi wetu wa Marekani. Mtu ninayemhurumia, katika taifa hili, ni Mhindi huyo. Hakika hawakupata haki kwake! Mimi si... Mimi ni mtu mmoja tu, bali ninawatetea. Naam, bwana. Kama Bwana kamwe akiniita kutoka hudumani, ya shughuli hizi, na ujumbe wangu umekwisha; Yeye akinijalia kuishi muda mrefu zaidi, nitaenda kwa Wahindi. Naam, bwana. Naam, bwana. Jamani!

²⁰⁷ Tunaona yale Amosi angefanya wakati alipopaza sauti. Mfumo wetu wote ungehukumiwa. Bila shaka sio...

²⁰⁸ Serikali haiwezi kujenga (tamshi langu lilikuwa) juu ya mwamba, ambapo taifa linapiga kura lipate mchanga.

²⁰⁹ Utalijengaje kanisa lako juu ya Mwamba? Mhubiri atasimamaje mimbarani kamwe na kuuhubiri Mwamba, na kulijenga juu ya kanuni za Injili yote, wakati kusanyiko lake, baadhi ya watu wake huko nje, wangemfukuza? Sasa, ninamlaumu mhubiri kwa kutokuwa na ujasiri, na Roho wa Mungu, kwa kuufunga tu mlango, aseme, "Tafuteni mtu mwingine atakayeutetea upuuzi huo na si mimi." Na—navutiwa na mhubiri ambaye angefanya hivyo.

²¹⁰ Lakini ole kwa kusanyiko hilo wakati mtu wa Mungu aliyetiwa mafuta anapojaribu kuwaletea Neno, halafu

hawatajinyosha na Hilo. Hiyo ni kweli. Atakuwaje na kanisa ambamo karama zote tisa zinatenda kazi ndani yake, na kadhalika, na halafu, wao na hayo, nalo kanisa hata—hata halitaishi kwa ustahifu na kwa maadili, hawatajifunza ABC zao za Injili? Kisha wanasema, “Laiti ningalikuwa na mhubiri bora zaidi!” Mbona, ni makosa yako. Hiyo ni kweli.

²¹¹ Ni kosa la taifa letu, Wamarekani wetu, kwamba tumekuja huku kwa ajili ya uhuru wa kuabudu. Kutoka kwa nini? Halafu tunarudi moja kwa moja, na kuweka kwenye makao yetu makuu kitu kile kile tulichokuja hapa tupate kuwa huru nacho.

²¹² Taifa hili linafanana kabisa na Israeli. Wao, Israeli, walikuja Palestina, wakawafukuza wenyeji na kuiteka nchi. Mwanzoni, walikuwa na watu wema—wema, juu yao. Walikuwa na Daudi, na Sulemani, na watu mashuhuri. Hatimaye, baada ya kitambo, wakaendelea kupiga kura mle, na kujisukumiza ndani, na kupiga kura mle, mpaka wakampata Ahabu kule chini, ambaye alioa kafiri. Sasa, Ahabu alikuwa ni jamaa mzuri sana. Ninii yake. . . Loo, a—alitaka kufanya mema, bali asingeweza kutenda mema, kwa ajili ya mwanamke huyo wake.

²¹³ Sasa, sina chochote dhidi ya huyo mtu niliyekuwa nikinena habari zake dakika chache zilizopita. Huenda akawa ni mtu mzuri. Bali ni mfumo huo wa huyo kahaba nyuma yake, unaoipindua shingo yake. Hicho ndicho kitu kitakacholisababisha. Anaingia kwa urahisi tu awezavyo, namna hiyo, na kukitupilia chini kitu hicho chote.

²¹⁴ Hivi mlijua sisi ni—sisi sasa ni. . . Deni yetu ya kitaifa ni kubwa mno, hata tunalipia pesa zilizokopwa, kutokana na kodi tutakazopata miaka kumi na minne kuanzia leo. Itakuwaje wakati mfumo huu utakapoporomoka?

²¹⁵ Castro, hakika, simuungi mkono. Yeye ni mkomunisti. Kweli. Simuungi mkono. Bali alifanya jambo zuri wakati alipobadilisha fedha na kurudisha dhahabu, akanunua hati za ukopeshaji na kuirudisha dhahabu.

²¹⁶ Itatulazimu kufanya hivyo, ama kuna kitu kimoja kilichobandikwa usoni mwetu, hicho ni, ya kwamba kanisa Katoliki linamiliki utajiri wa ulimwengu. Lina pesa. Linazo dhahabu, kununua hati zetu za ukopeshaji tena. Hiyo ni kweli kabisa. Nanyi mnafikiri hawa wauza wiski, na wauza tumbaku, na watu mashuhuri wa humu nchini hawatatusaliti, wasije wakapoteza biashara zao zote na kughushi fedha? Watarudi moja kwa moja nyuma na kuchukua fedha hizo kutoka kwa kanisa Katoliki, na ndipo limejiuza kabisa. Kweli. Hivi Biblia haibashiri hilo, “Utajiri wa ulimwengu”? Mimi si mwanasiasa, wala mtu mwerevu, bali namshukuru Bwana ninamjua. Na hiyo ni kweli. Hapo ndipo litakapokaa, papo hapo. Ninyi liangalieni. Ninyi angalieni muone kama hiyo si kweli. Ninii

tu...Natumaini sote tutaishi tupate kuliona, nami sidhani itatubidi kuishi muda mrefu sana.

217 Lakini mtafanyaje? Tutajengaje kanisa? Tutajengaje taifa? Tatalijengaje taifa juu ya hili sasa? Tutaifanya nini juu ya jambo hilo?

218 Labda afadhali nifunge domo, niende mahali pengine. Lakini, mwajua, nimesema ya kutosha hata mnajua ninalozungumzia. Mnaona? Mnajua ninalomaanisha.

219 Angalieni kile tunachotaka. Ninyi, mnaona mnachotaka? Hicho ndicho mnachopata. Hizo ni shauku zenu.

220 Angalieni vipindi vyetu vya televisheni siku hizi, visivyokaguliwa. Ilikuwa kwamba, ilikuwa kosa kwa watoto wetu, tusingewaruhusu kushuka m—mjini kuona sinema, ma—maonyesho ya sinema. Lakini sasa ibilisi aliligeza hilo moja kwa moja na—na kuifanya televisheni, na kuiweka katika kila nyumba.

221 Na hilo lingekuwa ni sawa, televisheni ni sawa, kama una kitu kifaacho ndani yake. Hakika, ni sawa.

222 Lakini mnaifanya nini? Inaendelea kuoza zaidi na zaidi kwa saa, wakilitumia jina la Mungu, wakiapa, wakilaani, wanawake walio uchi, matendo machafu, ambayo huitia sumu akili ya watoto hawa, mpaka tumelilea kundi la wapinga maadili, hiyo ni kweli, majambazi wa kutisha. Ni kweli hasa. Afadhali mliangalie.

223 Taifa letu lote linageuka kuwa kundi la majambazi wa kutisha. Mvulana yeyote anayetembea huku suruali zimening'inia kwenye nyonga zake, na kichwa kimeinama nyuma, na nywele zake zimening'inia shingoni mwake kama mkato kichwa-maji wa nywele wa Bibi Kennedy, na akizunguka namna hiyo, kama jambazi la kutisha, halafu mnamwita huyo Mmarekani? Mmeanguka kutoka kwa neema. Tubuni mkamrudie Mungu, la sivyo mtaangamia. Hiyo ndiyo sababu, tu—tunataka kumleta mtu fulani humu ndani ambaye ataturuhusu kufanya lolote tutakalo. Hiyo ni kweli.

224 Hivyo ndivyo ilivyo na makanisa. Wanataka kumchagua mchungaji, sio mchungaji ambaye atasimama pale na kuwashindilia Injili. Lakini wanataka mtu fulani ambaye atawaruhusu wajinyoshe katika suti ya kuogelea, na kucheza mchezo wa karata kwenye orofa ya chini, na kuishi vyovyote watakavyo, vipindi vya televisheni vya radio isiyokaguliwa, uchafu na takataka, kuunganisha kanisa na ulimwengu pamoja.

225 Si ajabu Amosi angeukemea upuuzi huo. Mnafikiri watu wangempokea wakati wao ndio waliokipigia kitu hicho kura wakakiingiza moja kwa moja ndani?

226 Kama mchungaji akihubiri zaidi ya dakika ishirini, halmashauri ya wadhamini wanamwita chumbani na kusema,

“Angalia hapa, mchungaji. Ha—hatukukuleta hapa kufanya jambo kama hilo. Tuna ratiba ya dakika ishirini. Hizo zikiisha, tuachilie tuondoke.”

²²⁷ Anachohitaji kufanya ni kulifukuza kundi hilo la wadhamini litoke nje, na kuchukua Biblia na kuhubiri usiku kucha, kama Paulo alivyofanya, apate kuona ufufuo wa wafu. Kweli kabisa. Wakimfukuza jengoni; pembeni mwa mtaa panafaa. “Mungu anaweza kutoka kwenye mawe haya . . .”

²²⁸ Televisheni, maonyesho ya sinema zisizokaguliwa, uchafu, kinyaa, nazo zinatoa mfano. Waangalieni watoto wetu wadogo siku hizi. Waangalieni wasichana wetu. Waangalieni maskini jamaa hao wadogo wanaotoka shuleni, si zaidi ya umri wa miaka sita, saba, nane, wakiwasha sigara. Mbona hivyo? Mama yao mbele yao labda alifanya hivyo. Kama hawakufanya hivyo, basi baadhi ya watoto wanaoshirikiana nao. Angalia ni nani watoto wako wanacheza naye. Kweli. Hapa hivi . . .

²²⁹ Wakati fulani uliopita, mke anajua hilo, tulikuwa tumeketi mezani. Ndipo mtoto wangu Joseph akafoka neno ambalo lingemfanya baharia mlevi ajionee aibu. Nikageuka. Nikasema, “Nini hilo?” Naye mama karibu azimie. Maskini jamaa huyo alionekana asiye na hatia.

²³⁰ Akasema, “Kuna nini, baba?” Na machozi makubwa machoni mwake.

²³¹ Nikasema, “Kamwe usiseme kitu kama hicho.” Hakujua hayo yote yalihusu nini. Tukaja kugundua, watoto shuleni walikuwa wakitumia neno hilo chafu. Nikasema, “Kipenzi, hilo ni la ibilisi.”

²³² Mnaona, wewe hapo, watoto wako. Imefikia tu mahali, ndugu, mpaka ni hali ya kutojali kabisa, mkusanyiko kama huo wa dhambi. Loo, jamani! Vipindi vya televisheni, wapenda dhambi, wapenda anasa! Loo, jamani!

²³³ “Dakika ishirini ni muda mrefu kutosha. Sina budi kuona kipindi cha mwisho.” Mnaona? “Harakisha na uondoe hili hapa. Sina budi kukiona.” Mnaona? Wametekeleza dini yao. Walishuka wakaenda huko chini, na hilo latosha.

²³⁴ Lakini, nawaambia, mwanamume halisi ama mwanamke aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu ataketi saa baada ya saa, akinywa kwenye Neno la Mungu. Si hayo tu, bali wakati linapogonga pale, linatia nanga na kubadilisha maisha. Amina. Naam.

²³⁵ Ni shauku ya watu wetu. Mpangilio wetu wote umepotoka na kuoza. Ni shauku za watu wetu.

²³⁶ Hebu mchukue mtu mzuri, tuseme, kama mwanamume mzuri, mweke katika familia ambayo ni kundi la wapenda anasa, watamdhalilisha mtu huyo; ama, mwanamke mzuri, mojawapo, uwaweke katika familia ambayo imechanganyikiwa. Mbona,

familia yote inapaswa kujisalimisha kwa Mungu. Ni kazi yetu kuomba, mpaka watoto wetu waoko, kuiweka nyumba yetu katika utaratibu. Naam.

²³⁷ Sisi ni kitu kama Israeli walivyofanya, waliofanya ushirikiano na adui zao. Kwanza, ilibidi watoke kwenye Neno kabla hawajaweza kufanya hivyo. Basi inaonyesha tu jinsi ambavyo Marekani imeliacha Neno.

²³⁸ Mnajua, i—inakubidi kukana ukweli kabla hujaweza kuamini uongo. Hiyo ni kweli. Hiyo ni hakika. Ilibidi Hawa kwanza kulikana Neno la Mungu kabla hajaweza kuchukua uongo wa Shetani. Iliwabidi kuondoka kwenye Neno wakati ule, vivyo hivyo sasa, kuuacha Urumi uchukue mamlaka pasipo kufyatua risasi hata moja. Wao hawalijui Neno la Mungu kuhusu mambo haya. Hiyo ndiyo shida yake.

²³⁹ Tunahitaji kutokea kwa nabii wa kweli, aturudishe kwenye Neno. Hiyo ni kweli. Tumeahidiwa mmoja. Tumeahidiwa hilo. Naam, hakika. Malaki 4 ilisema atatokea. “Naye angeirudisha Imani ya watu iwarudie hao baba wa kipentekoste tena.”

²⁴⁰ Amosi alijua ya kwamba wapenzi wa Israeli makafiri siku moja wangewaangamiza. Sasa hebu niseme hili kwa uchaji. Vivyo hivyo mwaminio leo hii anajua ya kwamba ulimwengu, hawa wapenzi makafiri wa Marekani, watamwangamiza. Kupenda kwenu siasa! Nitaliacha hilo likolee kwa dakika moja. Huko kutaliangamiza taifa. Na kupenda kwenu ulimwengu, kutokuja na Neno na kujaribu kufanya yaliyo haki, kutaliangamiza kanisa. Hiyo ni kweli kabisa. Natumaini hilo limekolea. Kanisa lilikuwa limemwacha, likaliacha Neno Lake la Uzima. Ulimwengu mzima hujikwaa kwake, kama jiwe la kujikwaa. Wanafanya jambo lilo hilo siku hizi. Naam. Kama Amosi alikuwa hapa, angeukemea huo mfumo wote.

²⁴¹ Sasa, katika kufunga, ninataka kusema hili, katika kifungu cha 8. Sikilizeni kwa makini. Yeye alisema, “Simba anaponguruma, ni nani asiyeweza kuogopa wakati simba anaponguruma?”

²⁴² Nami nimewawinda simba. Simba ni mfalme wa wanyama. Huko Afrika nimelala kule kwenye majangwa hayo, usiku, chini ya hizo nyasi chache, ama ilikuwa ni vichoma nguo.

²⁴³ Simba ataruka moja kwa moja mbele ya bunduki inayopiga. Haogopi hiyo, bali hataukaribia mwiba. Mmesikia ile hekaya. Lakini, hiyo ni ya kweli, simba hataukaribia mwiba. Wanajenga vibanda vya miiba namna hiyo, na simba hatakirukia. La sivyo, angepata, angeingia moja kwa moja ndani.

²⁴⁴ Mimi pamoja na Billy. Ninakumbuka tukilala kule usiku mmoja, na kusikia maskini kinywa chake kikubwa kikipitia hapo karibu, umbali *huo* kutoka kichwa changu, mnaona, ila a—asingekaribia. Wayo wake mkubwa, karibu namna *hiyo*, akitembea hapo karibu ardhini.

245 Nawe unaweza kusikia kila kitu kuanzia fisi, fisi waanguao kicheko, fisi waliao, na—na wao—wanapiga makelele. Halafu—halafu unawasikia nyani, tumbili, na—na twiga, na ndovu wakiwa na milio hiyo mikuu na “whiii.” Unaweza kuwasikia kwa maili kadhaa. Na wadudu na mende wa kila namna wakupiga kelele zao. Lakini hebu tu simba angurume kwa mbali, hata mende wanaacha kupiga kelele. Wanasikiliza. Kwa nini? Ni mfalme wao. Wanamsikiliza.

246 Biblia ilisema, “Wakati Mungu... Simba akinguruma, ni nani asiyeuweza kuogopa? Basi Mungu anaponena, tunawezaje kukosa kutabiri?” Tunaweza kujiepusha nako? Mungu anaponena, nabii hulitangaza Neno lililonenwa kwa sauti. Na kama ni Neno la Mungu... .

247 Naye simba anaponguruma; mende, kila kitu, hutulia, kwa sababu wanaogopa. Mfalme wa—wa—wao a—anzungumza. Wanayo a—akili ya kutosha, ujasiri, na heshima ya kutosha, kumheshimu mfalme wao anaponena.

248 Kwa hiyo, Mungu hunena kwa Neno Lake, basi kila kiumbe cha uumbaji Wake na kitilie maanani. Yeye ananena katika siku hizi za mwisho. Yeye anatoa Neno Lake. Basi kila kiumbe ambacho ni cha Ufalme Wake na kitilie maanani yale anayosema. Kisimame. Kijichunguze. Yeye ananguruma sasa, ananguruma kwa Neno Lake lililothibitishwa. Anajitambulisha Mwenyewe. Wakati anaponguruma katika siku hizi za mwisho, na tutilie maanani, na kujua ya kwamba kuna jambo fulani lililo karibu kutukia, tukijua ya kwamba Mungu kamwe hafanyi jambo hilo pasipo kunguruma kwanza. Wakati anaponguruma, basi kitu fulani kinafuata mngurumo huo, naam, kwa kuwa Yeye anajitokeza basi.

249 Yeye alisema, “Hivi ninii—ninii... Hivi simba hunguruma sasa pasipo na sababu? Simba mdogo hulia, kutoka pangoni, kabla hajapata chochote?” Mnaona?

250 Mungu ana sababu ya kunguruma, kwa sababu anajua kwamba hukumu imekaribia. Na, Neno Lake, Neno Lake ni nabii. Ndivyo alivyo. “*Hili* ni unabii wa Yesu Kristo.” Ni ufunuo, Mungu akijifunua Mwenyewe kwetu kupitia Neno Lake lililoandikwa. Na Yeye ni Neno. Na, sasa, *hili* ni Neno Lake. Hakuna kitu kinachoweza kuongezewa Kwake wala kuondolewa Kwake, bali halina budi kuishiwa na kunyoshwa jinsi tu lilivyo. Haitupasi kuthubutu, kuondoa chochote Kwake wala kuongeza chochote Kwake. Mungu angali ni Mungu. Yeye ananguruma.

251 Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu. Walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, wakiolewa, utovu wa uadilifu.”

252 “Na kama ilivyokuwa katika siku za Lutu,” Yeye alikuja Mwenyewe katika mwili wa nyama, na kujithibitisha

Mwenyewe kwamba yupo hapo kwa Ibrahimu. Kasema, “Ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Yatazameni mambo haya. Nuru za jioni zinaangaza.

²⁵³ Loo, kama tulikuwa na Amosi jukwaani leo hii, tumwache angurume, angeilipua mifumo yetu na mapokeo yetu, nalo Neno la Mungu lingesonga mbele kwa ushindi.

Na tuombe.

²⁵⁴ Baba wa Mbinguni, nena tena. Nguruma, Bwana, kwa Roho Mtakatifu. Yeye ndiye Nabii wa wakati huu. Yeye ndiye Nabii wa siku hii, akijaribu kupata njia Yake kuingia mioyoni mwa wanaume na wanawake, ili aweze kusema Kweli. Nina furaha sana kwamba anawapata wengine. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba Yeye atawapata wengi hapa ndani usiku wa leo, ili aweze kumtumia mtu aliye tayari kuwa na uchaji. Wanapousikia mngurumo wa mwenyezi Mungu ukitokea kwa Neno Lake, hukumu imekaribia.

²⁵⁵ Simba anaponguruma, yeye yuatokea. Kila—kila kiumbe kinajua afadhali kijifiche, kwa sababu mfalme anasogea.

²⁵⁶ Mungu, tuna eneo moja tu la usalama, wakati Mfalme wa wafalme anaponguruma, hilo ni Damu ya Yesu Kristo. Tunalo eneo la usalama. Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utanena na mioyo usiku wa leo. Na uwajalie kujua ya kwamba wanaishi katika vivuli vya Kuja kwa Kristo, wakati mataifa yanavunjika, na mambo yanaendelea, ya vile yalivyo. Na, hata hivyo, katika rehema Zako zenye huruma . . .

²⁵⁷ Tumetenda dhambi sana, inaonekana kana kwamba ungetupa kisogo, na kutuacha tuondoke. Lakini, hata hivyo, kama ulivyokuwa huko nyuma Edeni, Wewe hufanya njia ya kuepukia. Ulifanya njia ya kuepukia kwa ajili ya Nuhu. Ulifanya moja kwa ajili ya Musa, na kwa ajili ya Danieli, wana wa Kiebrania. Wewe, sikuzote unafanya njia. Nao wale wanaoipata, wanatembea katika Nuru ya Mungu na wanapata Uzima. Wale wanaoikataa Hiyo, wanahukumiwa na kutupwa mbali.

²⁵⁸ Ninaomba, Baba wa Mbinguni, hakutakuwako hata na mmoja wa hao usiku wa leo, waliotupwa mbali. Naomba kwa utamu wasikie mngurumo wa Mungu, Roho Mtakatifu akinena ndani ya mioyo yao, na kusema, “Huyu ni Mimi. Msiogope. Ni Mimi.” Kwa kuwa tunaomba hayo katika jina la Yesu. Amina.

²⁵⁹ Nitausimamisha wito wa madhabahuni kwa yapata dakika kumi. Nimechelewa kidogo. Lakini ninaamini Billy alisambaza kadi za maombi siku chache zilizopita usiku, ama kitu kingine, huko kwa Ndugu Groomer. Pia nafikiri amekuwa akizisambaza jana usiku. Kamwe sikuwaita. Sininii. . . Nadhani alizisambaza tena usiku wa leo. Sijui kama alifanya hivyo ama hakufanya, lakini hebu tuite baadhi ya kadi hizo. Ndugu Groomer yuko hapa? Groomer? La, la. Groomer. Yuko hapa? Tulianza wapi?

Kuanzia kwenye namba...Hivi hatukuanza kwenye namba moja, huko juu?

²⁶⁰ Jana usiku, hatukuwa na kadi za maombi. Sisi...Roho Mtakatifu alienda tu moja kwa moja kupitia kwa wasikilizaji na kuwaita watu. Mnapenda hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ninalipenda, pia. Na kuhubiri kwa nguvu namna hii, hiyo huenda ikawa kidogo sipendi hilo.

²⁶¹ Ni—nikiwapa watu kadi ya maombi, ninawajibika kumwombea mtu huyo. Hivyo tu. Endapo hatuna utambuzi wowote, hilo ni sawa. Lakini ninawajibika kumwombea mtu huyo. Mwanangu akitoa kadi ya maombi, si—sina budi kumwombea mtu huyo. Hivyo tu. Kwa hiyo, na—najisikia hivyo. Nitawaombea, Mungu akinisaidia. Kabla sijaondoka nchini humu, nita—nitawaombea.

²⁶² Sasa, hatuwezi kuchukua muda mrefu sana. Hebu tuone, tulianza kutoka moja hadi ishirini na tano, ninaamini ndivyo ilivyokuwa, usiku huo. Naam, moja hadi ishirini na tano. Mimi...Ndugu Groomer, uko hapa? Ndugu Groomer? Silitamki hilo vizuri. Lakini nafikiri hilo ni sawa. Moja...

²⁶³ Vema, hebu tuanze mahali pengine usiku wa leo. Hebu tuanze, hebu tuanze kutoka sabini na tano, basi, hadi mia moja. Ni nani aliye na kadi ya maombi namba sabini na tano, inua mkono wako. Hebu tuone kama...Vema, hiyo ni kweli. Hilo ni jema. Vema, njoo hapa juu, mama. Sabini na tano, sabini na nne, sabini na...sabini na tano tu. Sasa sabini na sita, sabini na saba, sabini na nane, sabini na tisa, themanini, themanini na moja, themanini na mbili, themanini na tatu, themanini na nne, themanini na tano, themanini na sita, themanini na saba, themanini na nane, kuendelea hadi mia moja. Acheni waje hapa. Billy Paul yuko wapi? Samahani. Sawa. Nenda, shuka pale chini. Hebu mabawabu fulani wamsaidie mpaka waingie kwenye mstari wa maombi.

²⁶⁴ Sasa, wengine wenu, niangalieni mimi kwa dakika moja. Naam. Hivi mnampenda? Hebu tuimbe kwa upole, utamu, kwa dakika moja tu, wakati baadhi yenu ninyi ndugu mabawabu mnaposhuka kule. Loo, asanteni. Wamewapata, huko chini, kwa hiyo wao...Kwa hiyo mistari hiyo haitavurugwa. Ninataka kuwaombea watu hawa. Halafu, kesho, labda tutakuwa tukiwaombea wagonjwa vivyo hivyo tu, na kuendelea na kuendelea, mpaka ule mkutano utakapoanza. Na mimi...

²⁶⁵ Huenda ikawa Ndugu Roberts atakuwa na mstari wa maombi kule juu, pia, huko juu ma—mahali pale. Nilikuwa nikiwazia labda sote wawili tuwe na mmoja pamoja, mmoja upande mmoja, na mwingine upande mwingine. Lakini si—sijui kama angependa hilo au la. Sijazungumza naye, na afadhali nizungumze naye kwanza, mnaona. Ndugu Oral ni ndugu mzuri, ni mtumishi halisi wa Kristo. Naye angekuwa mnyenyekevu vya

kutosha kufanya hivyo, bali kidogo ninachukia kujitupa mle pamoja na mtu kama huyo, mnaona. Kwa hiyo labda afadhali niliache tu. Vema, kama angeniambia, kama angeniomba, “Ndugu Branham, njoo unisaidie,” ninge—ningefurahia kufanya hivyo. Lakini, sasa, yeye ni mnyenyekevu na ndugu wa kupendeza sana. Na kama angeniomba kufanya hivyo, mimi, hakika, ningefanya. Lakini ningetaka yeye aniombe, kwanza, mnaona. Afadhali nisiseme kitu juu yake. Msilitaje kwake, sasa. Acheni—acheni tu yeye aniombe, ndipo nitajua ni sawa. Mnaona?

²⁶⁶ Lakini sasa—sasa tutaona. Ni wangapi wanachukua... Vema, sasa, hebu tuone. Ni kadi ngapi za maombi zilizo humu jengoni? Hebu tuone mikono yenu. Loo, kuna kiasi kikubwa zaidi, labda hamsini zaidi. Arobaini, hamsini zaidi, labda. Loo, naam, labda thelathini zaidi. Vema. Sasa tutapata—tutapata...

²⁶⁷ Tutazipata. Sasa tutaninii... Ishikilie tu kadi yako, ikiwa hujaitwa. Unaona, ni saa nne na dakika kumi, na mimi—mimi ninawataka mwe kwenye shule ya Jumapili asubuhi. Na labda kesho, tukiwa na ibada mbili, huenda tukamalizia karibu kadi zote tulizo nazo basi, halafu—halafu tuanze upya kwa ajili ya Jumatatu tena.

²⁶⁸ Tutakuwa wapi Jumatatu usiku? Loo, tuko chini, tuseme, huko Tucson. Msisahau kuja huko chini Tucson sasa, kwenye ule mkutano kule chini. Mtu yeyote hapa kutoka Tucson? Naam. Hakika. Eneo la Shamba la ulimwengu, bila shaka, mnapaswa mwe mmetoka huko. Ndugu Carl Williams ataniandama kwa sababu ya hilo, moja ya siku hizi. Nilipokuja hapa kwa mara ya kwanza, ilikuwa ni miji shindani, nami ninaona ingali hivyo.

²⁶⁹ Nimezoea hilo. Mpira wetu, timu yetu ya besiboli, ama ya mpira wa vikapu huko nyumbani, hiyo ni miji shindani, Jeffersonville na New Albany, loo, jamani, jamani, jamani! Whiu! Kama kuna usiku ambapo hamna mapambano makuu, wanapokuwa na mchezo, basi sijui mahali ingeweza kuwa.

²⁷⁰ Wao sikuzote wanashindana, ninajua, huko Tucson. Lakini Phoenix imepanuka kushinda Tucson mara nyingi, ninaamini, maana mimi... Tucson, sidhani ni theluthi moja ya ukubwa wa Phoenix. Lakini...

²⁷¹ Tunashuka kule, maana wanao watu wazuri watakatifu, kule chini, nina hakika. Kila mahali nimeenda ulimwenguni, hata kwenye misitu ya Afrika, ningali ninawapata. Loo, jamani! Laiti ningemfanya mke wangu aje huku juu na kuwambia wimbo huo usiku mmoja, “Wanakuja kutoka Mashariki na Magharibi, kutoka nchi za mbali.” Sasa, yeye atasimama na kuponyoka atoke nje wakati niliposema hilo.

²⁷² Kwa hiyo, yeye anamwogopa Ndugu Rose hata kufa. Ndugu Rose alisema, “Dada Branham yupo hapa. Tunamwalika apande huku, akaseme neno.”

273 Akasema, “Moyo wangu uliruka karibu miruko kumi na mitano.” Kasema, “Nikainamisha kichwa changu chini upesi.” Kasema, “Bill, ikiwa yupo mahali popote mkutanoni,” kasema, “hakika nitajificha.” Yeye ni mshamba kweli. Kwa hiyo, ni—ni—nitasikia kutokana na hili nitakapofika nyumbani.

274 Ninatumaini ya kwamba ninyi vijana wote...Ninasema hili, si kwa sababu yeye yupo hapa. Mnajua hivyo, na wote wanaomjua. Natumaini ya kwamba kila kijana mwanamume humu jengoni, wakati atakapomwoa mke wake, kwamba yeye ni mzuri jinsi hiyo kwake, nanyi mna furaha pamoja, kama mimi na mke wangu tumekuwa miaka hii yote. Iwapo kuna heshima yoyote itakayotolewa kwa familia ya Branham, na imwendee. Yeye ni malkia. Hakika ni malkia. Kwanza, yeye ni mama halisi. Halafu angalieni yale imembidi kuvumilia, mnaona, halafu basi, vema, mnge—mngeshangaa hayo ni nini. Mbona, watu mlangoni, usiku na mchana. Naye husimama kati yangu na umma, mnaona, hapo ndipo, nyumbani. Kwa hiyo hiyo kweli ni kazi ngumu.

275 Naye maskini Billy Paul, ninawazia, mara nyingi, nilimbeka kote, wakati mama yake alipokufa, maskini mtoto mchanga. Dk. Adair alizoea kusema, “Wewe ni jamaa wa kipekee.” Nami ningekuwa huko chini mtaani, nimembeka, huku akimlilia mama yake, huku hali ya hewa ni baridi, mwajua, mimi nikimshikilia begani mwangu, namna *hii*.

276 Na sikuwa na pesa za kutosha kuweka ninii yake... ama kumnunulia chupa halisi. Nilimnunulia chupa ya Koka yenye chuchu juu yake. Ningeiweka *hapa*, na kuiweka kwapani mwangu, idumishe joto. Akilia kupita kiasi, ningenyosha mkono, niingize hiyo chuchu kinywani mwake. Nimwache anyonye muda kidogo, kisha nikairudishe hiyo chupa *hapa* chini. Nami nilikuwa nimelowa maziwa mwili mzima, na kila kitu, mwajua.

277 Nilikuwa nikimshikilia, nikisonga mbele moja kwa moja, mwajua, nikimbeka. Usiku, jamani, jamani, jinsi nilivyojaribu kumpembeza apate kulala, na kumtafuta mtu aje amwangelie wakati nikienda kuwaombea wagonjwa. Tumetoka mbali pamoja. Natumaini Yeye atatudumisha hivyo.

278 Nilimwona jana, akimbeka mvulana wake mdogo. Nami nikawaza, “Billy, huyo alikuwa ni wewe, muda mfupi tu uliopita.” Vema, hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya, kuondoka njiani, na kuwapa wengine nafasi. Jina la Bwana libarikiwe.

279 “Simba anaponguruma, mnaona, ni nani asiyeweza kuogopa?” “Na kumcha Mungu ni chanzo cha hekima.” Hiyo ni kweli? Hivyo ndivyo yule mtu mwenye hekima alivyosema. “Kumcha Mungu.”

280 Sasa, ninawatakeni ninyi watu kwenye mstari huo wa maombi, mnaosimama hapo, ninyi nyote mnaojua ya kwamba sijui lolote kuwahusu, inueni mikono yenu. Kila mmoja. Bwana mwema wa Mbinguni akiwa ndiye Hakimu wangu; kadiri

nijuavyo mimi maishani mwangu, sijawahi kumwona mmoja wao maishani mwangu. Huenda ikawa wao wameniona, wakiwa wameketi kwenye wasikilizaji.

²⁸¹ Sasa, ni wangapi huko nje kwenye kusanyiko, wanaojua ya kwamba sijui jambo moja kuwahusu? Lakini, hata hivyo, wewe ni mgonjwa, nawe unaamini ya kwamba, Mungu, ungeweza kugusa upindo wa vazi Lake, na Mungu angesema nami nikuite, kama alivyofanya yule mwanamke, kama yule mwanamke asilia? Loo, jamani! Si ajabu nilihubiri kwa muda mrefu sana. Kusanyiko kama hilo, likiwa na imani ya aina hiyo, linapaswa kufanya hivyo.

²⁸² Huyu ndiye yule mama? Sasa, huyu hapa mama mmoja. Tunakutana usiku wa leo kama wageni, na sasa yeye anasimama hapa. Hakika, labda yeye ni mgonjwa, ama huenda akawa na shida nyingine.

²⁸³ Mnaona, Mungu hufanya mambo mengine mbali na kuwaponya wagonjwa, mnajua. Na kwa hiyo... Naye aliahidi kukidhi mahitaji yetu yote, mahitaji yetu, wakati mwingine si matakwa yetu, bali mahitaji yetu. Sasa nawatakeni ninyi kutafakari tu, moja sasa, mtakapoenda nyumbani, ama kama hamjapata kulisoma hapo kabla, mkasome Yohana Mtakatifu 4, ndipo—ndipo mwone sasa. Sasa, hapa, sasa, sikumbuki...

²⁸⁴ Hebu niseme hili. Ninaamini, huduma hii, ama ni kwamba Yeye anaenda kunipeleka nyumbani ama itapanda. Ni—ni moja kwa moja kufikia kwenye wakati huu wa mwisho. Au, ama anitume katika nchi za ng'ambo ama mahali fulani ambapo hawajawahi kulisikia. Mnaona? Kuna jambo fulani lililo karibu kutukia. Ninyi kumbukeni tu.

²⁸⁵ Pia, sikilizeni, mimi si mwuza kanda. Bali ninaye ndugu mzuri hapa anayezinasa kanda hizi, na huyo ni Bw. Maguire. Ninaamini ni James Maguire. Naye baba mkwe wa—wake, Ndugu Sothmann huko nyuma, wanazo kanda hizi. Ningependa, iwapo yeyote wenu ana kinasasauti... Sitasema lolote kulihusu sasa, maana sijui lolote kulihusu. Lakini kama uliwahi kununua kanda kutoka kwao, nunua kanda hiyo, *Mabwana, Ni Wakati Gani?* Isikilize, *Mabwana, Ni Wakati Gani?* Ichezeni kwa maombi, na ndipo mtaanza kuniombea. Mnaona? Wakati wewe... Maana, mtaona basi ni—nimesimama kwenye hatari gani papa hapa usiku wa leo. Nena kuhusu hatari, laiti mngalijua mahali nilipokuwa nimesimama, sasa hivi, papa hapa! Mnaona? Lakini sina budi kuendelea. Mshindi hatoroki, naye atorokaye hashindi. Hiyo ni kweli. Sina budi kutekeleza yale nimehubiri. Mnaona? Sasa, ninamwamini Mungu. Ninamwamini sasa hivi.

²⁸⁶ Sasa, hapa ni juu ya msingi fulani. Sasa, kama mimi—kama mimi nilikuwa Bwana wetu Yesu nimesimama hapa, naye mwanamke huyu alikuwa ni mgonjwa, mnajua nisingeweza kumponya kama ningalikuwa Bwana Yesu. Nisingeweza

kumponya, maana tayari nilikuwa nimeponya. Sasa, ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaona? Bila shaka.

²⁸⁷ Yeye tayari amesamehe kila dhambi. Tayari amemponya kila mgonjwa. Tayari ameitenga Damu hiyo pale Kalvari. Gharama tayari imelipwa. Yote imelipwa. Lakini jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuikubali Hiyo, kuiamini Hiyo na kuikubali. Wala huwezi kuikubali Hiyo mpaka kwanza uiamini. Unaona? Iamini Injili.

²⁸⁸ Sasa, lakini vipi kama Yeye alikuwa amesimama hapa, amevaa suti hii ambayo Bwana mwema aliwajalia Ndugu na Dada Williams kuninunulia, yapata miaka mitano ama sita iliyopita? Na vipi kama Yeye alikuwa amesimama hapa kwa ajili ya suti hiyo, ameivaa suti hii, naye mwanamke huyu alikuwa amesimama hapa?

²⁸⁹ Sasa, kama alikuwa na makovu mkononi Mwake, Yeye angesema, “Unaona, Mimi ni Masihi. Mimi... Mnaona haya makovu? Tazameni paji la uso Wangu.” Sasa, mwigaji yeyote angeweza kufanya hivyo. Hiyo ni kweli. Tusingemjua kwa hayo. Na kama Yeye alikuwa amesimama hapa namna hiyo, ningejua haikuwa ni Yeye. Ningejua siye.

²⁹⁰ Maana, Yeye atakapokuja, baragumu italia. Tutaninii... Yeye hata hatakuja duniani. Tutanyakuliwa juu hewani, kukutana na Yeye. Mnaona? Tutampata hewani. “Sisi tulio hai na tuliosalia tutanyakuliwa pamoja nao, kukutana na Bwana hewani.” Yeye haji kamwe duniani. Tunakutana na Yeye hewani.

²⁹¹ Lakini sasa, Yeye alisema, “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ukamilifu wa dahari. Kamwe sitawaacha wala sitawapungukia.” Anawezaje kuwa? Uzima Wake. Halafu, kama Uzima Wake ungekuwa ndani yangu, ndipo basi ningekuwa nikimwakilisha Yeye. Halafu, kama ungekuwa, ungekuwa ni Uzima ule ule uliokuwa ndani Yake, ungefanya mambo yale yale aliyofanya Yeye.

²⁹² Sasa, huyu hapa mwanamume na mwanamke, kama vile Yohana Mtakatifu 4. Yeye alikutana na mwanamke. Hakuwa amemwona hapo awali. Mwanamke hakuwa amemwona Yeye. Nao hao hapo wamesimama, pamoja. Ndipo akamwambia, yule mwanamke kisimani, kilichokuwa shida yake. Ndipo alipofanya hivyo, mwanamke alisema, “Bwana, naona kuwa Wewe ni—Wewe ni nabii.” Akasema, “Lakini tunajua ya kwamba Masihi, atakapokuja, Yule aitwaye *Kristo*, linamaanisha ‘Yule aliyepakwa mafuta’; atakapokuja, Yeye atafanya mambo haya, atatwambia mambo haya.”

Naye akasema, “Mimi Ndiye, ninayesema nawe.”

²⁹³ Sasa, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele; ila tu, mwili wa nyama... Yeye hutumia mwili wetu. “Yeye ni mzabibu. Sisi ni matawi.” Basi, Roho huyo angetenda tena

vile vile hasa alivyotenda alipokuwa ndani Yake. Hiyo ni kweli? Ingekufanya uamini? Sema, “Amina,” kama ingekufanya. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

²⁹⁴ Sasa, mama, mimi nikiwa sikujui, sijawahi kukuona maishani mwangu, nijuavyo mimi. Hakika, huenda umeniona barabarani ama katika mikutano, na kadhalika. Lakini hii ndiyo mara yetu ya kwanza kukutana.

²⁹⁵ Sasa, kama—kama uponyaji ndio unaohitaji, vema, mimi, kama ningaliweza kukuponya, ningekuponya, na kama nilikuwa na njia yoyote. Na iwapo ni pesa, kama ni—ningeweza kukusaidia, ningekusaidia. Na kama ungesema, huenda ikawa ni mtu mwingine, ungesema, “Nimekuja hapa, Ndugu Branham, upate ku—kumwombea mwanangu, ama binti yangu, ama dada yangu, ama baba,” ama mtu fulani. Ningefanya hivyo, unaona, chochote ningaliweza.

²⁹⁶ Na—na ikiwa ulikuwa na tatizo la kinyumbani, ningesema, “Ningetaka kukutana na wewe na mume wako, pamoja, na kuzungumza nanyi mahali fulani mbali na hapa, unaona, kusudi niweze kuzungumza nanyi nyote wawili nione mahali kosa lilipo hasa.” Halafu, wakati Roho Mtakatifu atakapofunua, aseme, “Ngoja kidogo. Ulifanya *hili* papa hapa wakati fulani *huu*.” Hilo latosha. Huwezi kukana hilo. Unaona? Aseme, “Ulifanya *hili* mahali hapa.” Halafu, basi limetatuliwa, unaona. Sasa, unaanza papo hapo. Unaona? Hivyo, imekwisha.

²⁹⁷ Sasa, unajua ninazungumza na wewe kwa kusudi fulani. Nimekuwa nikihubiri. Unaona? Halafu basi nina—ninajiweka mwenyewe katika—katika upako kwa ajili ya jambo lingine, unaona, kuona kama Roho Mtakatifu atakuja na kutenda kazi juu yangu kwa karama ya Kiungu; hiyo ni kusema, hizo dhamiri mbili zikikaa moja kwa moja pamoja, ambapo inanipa neema ya Mungu kuona maono, na kuona yanayotendeka, yale yatakayotendeka, yale yamekuwapo.

²⁹⁸ Utajua kama ni kweli ama si kweli. Umesimama hapa mbele ya angalau watu mia tano, unaona, ama karibu na hiyo, mia tatu, haidhuru. Unaona? Na—na unajua ya kwamba ni—ni. . . Unajua kama ni kweli ama si kweli. Na—na kama ni kweli, basi ni Mungu. Biblia ilisema, “Kukiwapo na mmoja miongoni mwenu, aliye wa kiroho ama nabii, na yale asemayo yanatimia, basi msikieni yeye.” Mnaona? Sasa, “Yasipotimia, basi msimsikie.”

²⁹⁹ Sasa, sina fununu mama huyu yuko hapa kwa sababu gani. Lakini sasa hebu Roho Mtakatifu aje, muone kama hataitaja. Mnaona? Na kama hilo halitakuwa ni jambo lile lile Bwana wetu alilofanya! Hilo tu ndilo angaliweza kufanya kama alikuwa amesimama papa hapa, maana, kumbukeni, ni Yeye. Ni Yeye. Sio mimi. Simjui. Ninakiri, simjui. Kwa hiyo, itahitaji Yeye.

Sasa, hakika, mama huyu kweli ana hisi ya ajabu kwa roho yake.

³⁰⁰ Si kwa sababu ameinua mkono wake. Nyote mmekuwa mikutanoni, na kuwaona wakiinua mikono yao, kufanya namna *hiyo*, naye Roho Mtakatifu anaita tena mara moja na kuwaambia kile walichokuwa. Mnaona? Hiyo ni kweli. Hilo halimaanishi chochote. Mmewasikia wakipiga mayowe na kupaza sauti; papo hapo, unawaambia papo hapo, “Unaishi na mke wa mtu *huyu*,” nililiona moja kwa moja *hapa*, na kila kitu kingine. Vema, mnajua. Mmekuwako mikutanoni na kuona jinsi mambo hayo, na kuona jinsi mambo hayo. Hilo halimaanishi chochote.

³⁰¹ Lakini mama huyo anaonekana kuwa na hisi ya ajabu kwa roho yake. Sasa, huyu mama anateseka na shida fulani. Ninamwambia, jinsi anavyokula. Yeye yuko mbele yangu sasa, mezani, na kidogo ana utaratibu wa maakuli ama kitu fulani, kidogo ni chakula cha kipekee. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? [Huyo dada anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Basi inua mkono wako ili watu wapate kuuona. Mnaona? Nilimwona huyo mama mbele zangu, akifanya jambo fulani. Chochote kile, liko kwenye kanda. Mnaona? Vema. Sasa, kusudi tu mpate kujua ni kwa sababu gani. . . Yeye ni mtu mzuri.

³⁰² Tazameni kwa dakika moja. Sasa Roho anatia upako. Sasa, kila mtu aketi kwa uchaji kabisa. Endeleeni kuomba. Iweni katika maombi, maana nimeiona ikienda juu ya kusanyiko papo hapo tu. Mnaona? Sasa iweni na kicho kabisa.

³⁰³ Hebu tumwone mama huyu tena, kuzungumza naye tu. Lolote alilokwambia. . . Naam. Hii hapa. Ni kwenye meza. Ni—ni ugonjwa wa tumbo. Na namna fulani ya maambukizi ama kitu fulani tumboni. Daktari amekuwa akiliangalia hili. Na, aisee, umekuwa na shida hii kwa muda mrefu. Na, wakati mmoja, ilitajwa, “Kidonda, kilichoibuka.” Na sasa alisema jambo fulani. Hiyo ilikuwa ni nini? “Duodeni. Duodeni. Duodeni,” Nilimsikia akisema hivyo. Mnaona? Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa. Jina lako ni Bi McCraw. Hiyo ni kweli. Endelea sasa, amini kwa moyo wako wote.

Mnaamini?

³⁰⁴ Baada ya kulia namna hiyo, akiketi kule nyuma, bwana, mapafu hayo yaliyokunjamana uliyokuwa nayo yanapaswa kusikia vema zaidi kufikia sasa, kama unaamini. Ni sawa sasa. Vema, hilo lilitosha. Amina.

Huyo aligusa nini?

³⁰⁵ Mwanamume, yapata wawili nyuma yake pale, aliye na ukakamavu wa arteri, kama unaamini pia, bwana!

³⁰⁶ Aligusa kitu gani? Hivi hamwezi kuona ile Nuru inayoning’inia pale? Angalieni hiyo Kaharabu *hapo*. Simjui mtu huyu, sijawahi kumwona maishani mwangu. Mwamini tu Bwana Yesu.

307 Sasa, mahali fulani, kuna maskini mtoto mchanga hapa, mtoto mchanga mwenye shingo kombo. Yule *pale*. Simjui. Amini, dada. Shingo ya mtoto huyo mchanga itanyoka, kama utaamini.

Yeye aligusa nini? Haleluya.

308 Kuna jambo lingine kuhusu shingo. Nililiona. Ni mwanamke. Siwezi kumwona. Naam. Ameketi hapa, akilia. Bibi Riley, mwamini Bwana Yesu Kristo, shingo yako itapona. Amini.

309 Simjui mwanamke huyo. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kumwamini Yesu Kristo. Mnaamini hilo? Iweni na imani.

310 Sikujui wewe, bwana. Sisi hatufahamiani mmoja kwa mwingine, kadiri nijuavyo mimi. Unaamini Yesu Kristo anaweza kuniambia shida yako ni nini? Unajua kama ingekuwa ni kweli ama si kweli, sivyo? Kama unaweza kuamini kwa moyo wako wote sasa! Inaendelea kwenda kwenye kusanyiko. Unaamini mke wako huko nje atapata afya, pia? [Ndugu huyo anasema, "Naam,"—Mh.] Ugonjwa wa macho, yeye anaugua ugonjwa wa macho. Unaamini hilo? Wewe hutoki hapa. La. Unatoka mahali palipo na maji mengi, njia fulani. Ni mji wa pwani. Ni California, Los Angeles. Rudi, Bw. Bowman, upate kupona. Naye Yesu Kristo atakuponya.

311 Mnaamini? Sasa, ninyi, kila mmoja anaweza kuponywa hivi sasa kama mtaamini. Mnaamini hilo?

312 Vipi kuhusu ninyi kwenye mstari wa maombi, mnaamini, pia? Iweni tu na imani, wala msitie shaka. Aminini kwa moyo wenu wote, dakika moja.

313 Mama huyu, sababu ya mimi kusimama pamoja naye, yuko katika hali mahututi. Mwanamke huyu atakufa mara moja kama jambo fulani halitendwi kwake, maana ametiwa uvuli. Mnaona ule uvuli mweusi juu yake?

314 Aisee, mnajua, tuna kivuli cha mauti hayo juu ya watu, kilichopigwa picha na kamera, kama tu yule Malaika wa Bwana? Tunachoonekana cheusi, kama kimbunga, kimening'inia juu ya mwanamke. Walimwambia asiipige hiyo picha. Naye Roho Mtakatifu akasema, "Ipige sasa hivi." Nao wakapiga picha, na kikawa ni hicho hapo. Mnaona? Pande zote mbili, hapa. Kimening'inia pale pale.

315 Ninyi watu mnaotoka maskanini, baadhi yenu ambao, mlio hapa, Ndugu Fred na hao wengine, hiki hapa kitu kile kile kimening'inia moja kwa moja juu ya mwanamke huyu.

316 Yuna kansa, hiyo ni kweli, kibofu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Mnaona? Sasa giza limeondoka, bila kusema lolote. Mnaona, imani yake tu, ndiyo

iliyofanya hilo. Nenda, ukiamini. Amina. Amina. Usitie shaka. Nenda tu na uamini kwa moyo wako wote.

³¹⁷ Ugonjwa wa moyo huwaua watu wengi, bali hautakuua kama utaamini. Amina. Nenda tu, ukisema, “Asante Bwana.” Nenda zako ukawe mzima. Vema.

³¹⁸ Ibilisi angekutaka uwe na hii baridi yabisi maisha yako yote. Lakini kama ukiamini kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakuponya. Unaamini jambo hilo? Anza kwenda zako, ukimshukuru Mungu.

³¹⁹ Unaamini kwa moyo wako wote? Unaweza kwenda ukale chakula chako cha jioni, nao ugonjwa huo wa tumbo utakuacha. Nenda tu na useme, “Bwana asifiwe!” Nenda, mwamini Yeye kwa moyo wako wote.

³²⁰ Ulikuwa, pia, na shida ya tumbo. Amini kwa moyo wako wote, kisha uende, naye Yesu Kristo atakupata afya. Vema.

³²¹ Unaogopa nini? Unasumbuliwa na wasiwasi. Karibu ukuvuruge kabisa, karibu uchanganyikiwe, Shetani akikudanganya. Lakini umekwisha sasa. Unaniamini mimi? Nenda, na useme, “Bwana asifiwe!”

³²² Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba utamponya dada yetu na kumfanya mzima, katika Jina la Yesu. Amina.

³²³ Njoo, ukiamini, dada. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaweka mikono yangu juu yake kwa ajili ya uponyaji wake.

³²⁴ Njoo, ndugu yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaiweka mikono yangu juu ya huyu ndugu kwa ajili ya uponyaji wake. Amina.

³²⁵ Ni wangapi walio na moyo unaoamini, chini ya mkono utakaoinuliwa? Sasa weka mkono huo juu ya mtu fulani aliye karibu nawe. Useme, “Amosi angesema hivyo?” Bila shaka angesema. Hilo ni Neno la Bwana. Wewe inua mkono wako, amini.

³²⁶ Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa...” Hata hakusema watawaombea. Alisema, “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, mkono tu ukiwekwa juu yao, watapata afya.”

Na tuombe.

³²⁷ Bwana Yesu, Mfalme amenguruma kwa Sauti Yake, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Bwana Mungu, jalia kila pepo apige makelele. Jalia kila maradhi yaondoke. Jalia ibilisi ashindwe, na watoto wa Mungu watoke kwenye jengo hili usiku wa leo katika ushindi na nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo.

³²⁸ Liamini. Hiyo ni kweli. Dumu tu moja kwa moja nalo. Sema, weka tu, weka mkono wako juu ya mtu fulani, ukisema, “Bwana, waponye.” Ninawatakeni muombe. Niliomba.

Nakutaka umwombee mtu fulani. Wewe ni—wewe ni . . . Wewe ni Mkristo kama nilivyo mimi. Sisi sote ni Wakristo. Sasa wewe mwombee mtu fulani. Wao wanakuombea.

³²⁹ Sasa, ungetaka mtu akuombee namna gani? Waombee kama vile ungetaka mtu fulani akuombee. “Watendee wengine, jinsi ungetaka wengine wakutendee.” Ombeni sana, iweni waaminifu, jinsi tu unavyowataka wakuombee.

³³⁰ “Nayo maombi ya imani yatamwokoia mgonjwa. Mungu atawainua. Na kama wamekuwa na kutokuamini kwokwote, kutaondolewa kwao.” Kwa nini? “Mfalme ananguruma. Ni nani awezaye neno ila kutabiri? Ni nani awezaye neno ila kushuhudia wakati Mfalme anaponguruma?” Neno Lake linasema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

Ndugu Fuller, njoo. Mungu akubariki.



MAPITO YA NABII WA KWELI SWA63-0119
(The Way Of A True Prophet)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumamosi jioni, tarehe 19 Januari, 1963, katika Hekalu la Imani huko Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org